

**Marioo usizunguke, sema ukweli tu**

UKURASA 20



**Solskjaer aitabiria makubwa United**

UKURASA 22


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 13, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580428

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**UNENE SI TATIZO**

**Ukijikubali kimavazi, utapendeza**

UKURASA 13

RIPOTI MAALUM

# Corona ilivyobadili maisha ya wanywaji pombe za kienyeji



UKURASA 4

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

WAZIRI ACHIMBA MKWARA MAMLAKA ZA MAJI

UKURASA WA 5

SERIKALI YAZINDUA MIFUMO UDHIBITI WA MATUMIZI HEWA


# ACT Wazalendo yatoa msimamo kuhusu Membe

UKURASA 2



UKURASA 2

Rais Wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akisalimiana na mmiliki wa Hoteli ya Park Hyatt kutoka Dubai, Ali Saeed Juma Albwardy, Ikulu za Zanzibar kwa ajili ya mazungumzo na ujumbe huo jana. Kulia kwake Yakoub Osman Sadiq. **PICHA: IKULU**

# Kasi ya Mwinyi siku 40 yatisha




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store



MICHEZO SIMBA, MBEYA CITY VITANI BARA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# ACT Wazalendo yatoa neno madai ya Membe kujiengua

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeibuka na kusema aliyekuwa mgombea wake wa urais kwenye uchaguzi mkuu uliomalizika hivi karibuni, Bernard Membe, bado ni kiongozi mwaminifu, tofauti na inavyojadiliwa katika mitandao ya kijamii.

Kimesema mkongwe huyo kwenye ulingo wa siasa nchini bado ni mwanachama wa ACT-Wazalendo, kwamba hajakiama. Membe ambaye alishiriki katika uchaguzi mkuu wa urais na wabunge uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, alipata kura 81,129 (asilimia 0.5) na kushika nafasi ya tatu mbele ya Rais John Magufuli wa CCm aliyeibuka mshindi kwa kupata kura 12,516,256 (asilimia 84) na Tundu Lissu wa CHADEMA kura 1,933,271 (asilimia 13). Baada ya kumalizika kwa uchaguzi huo ziliibuka taarifa katika mitandao ya kijamii kwamba mwanasiasa huyo na mwanadiplomasia mkongwe ameachana na chama hicho.

Nipashe ilimtafuta Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Dorothy Semu, ili kujua ukweli wa taarifa hizo ambaye alisema si kweli kwamba Membe ameachana na ACT- Wazalendo.

Semu alisema licha ya Membe kutozungumza chochote tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu, lakini bado anatoa ushirikiano mkubwa ndani ya chama.

"Kumbuka mgombea wetu (Bernard Membe) ni kiongozi katika chama pia ni sehemu ya Kamati ya Uongozi, ni sehemu ya Kamati Kuu, hivyo tunaendelea kushirikiana naye vizuri" alisema Semu. Membe ambaye aliwahi kuwa kada wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alitangaza kujiunga na ACT-Wazalendo Julai 15, mwaka huu.

Mjadala uliokuwapo katika mitandao ya kijamii kuhusu ukimya wa Membe unakuja kutokana na historia ya viongozi wakubwa kutoka CCM waliowahi kujiunga na vyama vya upinzani katika nyakati za uchaguzi mkuu, lakini miaka michache baadaye walitangaza kurejea katika chama hicho tawala.

Mmoja wa makada hao ni aliyewahi kuwa mgombea urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Edward Lowassa, ambaye miaka michache baada ya kumalizika kwa uchaguzi alitangaza kurudi CCM.

Mwingine ni Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, ambaye alihamia CHADEMA pamoja na Lowassa wakati huo lakini naye alirejea CCM, mwaka jana, ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kurejea kwa Lowassa kwa kile alichodai kuwa ni kukosa mwelekeo kwa chama hicho.

Hata hivyo, Membe bado hajajitokeza hadharani tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kueleza msimamo au maoni yake kuhusiana na uchaguzi huo.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Resty Mwasha (aliyenyoosha mkono kushoto), akipata maelezo kutoka kwa mwezeshaji mwenza wa mradi wa uchumi unaotekelezwa na Shirika la Tusonge CDO, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Winnes Munuo (kulia), akieleza jana namna walivyojikita kwenye sekta ndogo ya kilimo hai ili kuongezea kipato na kuhamasisha ulaji wa vyakula visivyokuzwa kwa kutumia mbolea za kemikali wakati wa mkutano mkuu wa tisa wa wadau. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Kasi ya Mwinyi yatisha siku 40

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, leo ametimiza siku 40 tangu alipoapishwa kushika wadhifa huo Novemba 2, mwaka huu.

Tangu aingie madarakani, ametawala vichwa vya habari kwa uamuzi anaochukua juu ya mambo mbalimbali ikiwamo kuwatumbua baadhi ya watendaji wa serikali akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Said Ndumbogani.

Pia katika siku hizo 40, Rais Mwinyi pia ameshawatumbua vigogo wawili wa afya, akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Ali Salum Ali na Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya, Jamara Taib.

Wakati wa kampeni, Rais Mwinyi aliwaahidi Wazanzibari kuwaunganisha katika mustakabali wa maridhiano ya kisiasa ambayo yapo kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar.

Wakati Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ilipotangaza matokeo ya uchaguzi na kumtaja mshindi, alipopewa nafasi ya kuzungumza Dk. Mwinyi, alisema yuko tayari kutekeleza maridhiano ya kisiasa na kuwakaribisha wapinzani katika serikali atakayoiunda.

**ZIARA BANDARINI**

Baada ya kula kiapo na kuingia madarakani, siku iliyofuata, Rais Mwinyi alianza kuchukua hatua muhimu kwa kuangazia maeneo muhimu ya uchumi, kwa kufanya ziara ya kushtukiza katika Bandari ya Malindi na kubaini msongamano wa makontena ya mizigo.

Inadaiwa kuwa msongamano huo wa makontena ulikuwa kero kwa wafanyabiashara hata kwa baadhi ya meli za mizigo kuchelewa kushusha mizigo.

Akiwa bandarini hapo, Rais Mwinyi alipata maelezo kuhusu kadhia hiyo kutoka kwa uongozi wa bandari lakini hakuridhishwa na utendaji kazi.

Watendaji hao walimweleza Rais Mwinyi kuwa moja ya sababu ya kuwapo kwa msongamano wa makontena ni kutokamilika kwa ghala la kuhifadhia mizigo, lililopo eneo la Sateni.

Akiwa bandarini hapo, Rais Mwinyi alilitembelea ghala hilo ambalo bado halijamalizwa kujengwa, licha ya serikali kukamilisha malipo yote kwa makandarasi wanaojenga jengo hilo.

Kutokana na hali hiyo, Rais Mwinyi alitoa maagizo ya kuanza kutumika kwa ghala hilo haraka, sambamba na kukemea tabia ya kufanya kazi kwa mazoea, kutokana na kampuni hiyo ya ujenzi kuchukua muda mrefu kujenga ghala hilo.

"Jambo hili halivumiliki kwani meli katika Bandari ya Zanzibar haziji na zinazokuja zinakawia kushusha mizigo hatua ambayo inatokana na uzembe na hatimaye kusababisha upotezaji wa mapato,"alisema.

Katika kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika bandari hiyo, Rais Mwinyi alifanya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari.

**ZIARA MNAZI MMOJA**

Baada ya kukamilisha ziara bandarini, Rais Mwinyi alifanya ziara katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, ambako nako alieleza kutoridhishwa na utendaji kazi hospitalini hapo. Hatua hiyo ilisababisha kumtumbua Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Ali Salum Ali, pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya, Jamara Taib.

Rais Mwinyi alifanya uamuzi huo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliofika hospitalini hapo, kuhusu kuzorota kwa utoaji huduma za afya, huku baadhi ya mashine muhimu zikiwa hazifanyi kazi.

**BARAZA LA MAWAZIRI**

Novemba 21, Rais Mwinyi aliunda Baraza la Mawaziri likiwa na Wizara 15, aliteua mawaziri 13 ambao aliwapa maagizo mazito 13, ikiwa ni kama dira ya utekelezaji wa majukumu yao.

Miongoni mwa majukumu ya msingi waliyopewa mawaziri hao ni kufuatilia miradi yote iliyotekelezwa katika wizara zao, kujua thamani halisi za fedha zilizotumika pamoja na kuangalia mikataba ya makandarasi wa miradi hiyo.

Pamoja na maagizo hayo, Rais Mwinyi aliitaka Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAEKA), kufanya uchunguzi wa miradi yote iliyotekelezwa, ili kubaini ubadhilifu wa fedha kwenye miradi hiyo.

Miongoni mwa maeneo muhimu ya uchumi ambayo Rais Mwinyi aliyataja kutoridhishwa kiutendaji ni Bandari na Uwanja wa Ndege.

Kauli hiyo, ilimlazimu Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, kufanya ziara katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na baada ya ziara hiyo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Ali Khamis alitangaza kutenguliwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ndumbogani.

Ndumbugani alitumbuliwa kwa kile kilichoelezwa kuwa kutofanya kazi kwa mashine za ukaguzi wa mizigo, hivyo kutoa mwanya wa upotevu wa mapato na dawa za kulevya kupitishwa.

HABARI KITAIFA

# Waziri achimba mkwara mamlaka za maji

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameanza kazi rasmi kwa kuwataka watumishi wa mamlaka ya maji watumie busara wakati wanakata maji kwa wananchi kwa sababu si wote wanaowakatia ni wasumbufu wa kulipa.

Akizungumza jana na watumishi wa wizara hiyo baada ya kuripoti ofisini kwake, Aweso alisema mamlaka za maji pamoja na jitihada za serikali kuwekeza miradi ya maji lakini lipo tatizo la watu kufanya kazi kwa mazoea.

"Lipo tatizo la watu kufanya kazi kwa mazoea yaani kuzoea shida za watu. Mwananchi wa kawaida anaweza kutuma ujumbe mfupi kwa mamlaka husika kwamba kuna bomba limepasuka na linatakiwa likazibuliwe ili waendelee kupata huduma, inawezekana hata huo ujumbe asijibiwe kabisa.

Aweso alisema mwananchi huyo huyo anajituma na wakati mwingine huchukua video fupi na kutuma kwa waziri au naibu waziri alafu kuongozi akiushusha kwa watendaji wa chini wanasema wameshafanyia kazi tatizo hilo.

"Uharaka ule ambao mnaufanya baada ya kuambiwa na kiongozi wako unashindwaje kuufanya kwa mwananchi ambaye ndiye bosi wako anayekusababisha upate mshahara?" alihoji.

Waziri huyo aliwataka watumishi hao wasizoee shida za wananchi na kuagiza wawasaidie kila wanapotaka huduma.

"Wakati mwingine mwananchi anakatiwa maji, siyo kwamba ni msumbufu kwenye kulipia bili ya maji yawezekana amepitia matatizo kidogo, wewe tu kwa sababu umeudhiwa na mkeo, unasema kata tu, zipo busara ambazo mnaweza kuzifanya.

"Hatusemi kwamba watu wasilipe bili za maji, mtu unaona ametumia maji na unamuona ni mkorofi kwa sababu tupo nao kila siku unachukua hatua lakini kuna wengine unasema hapana, tutengeneze mahusiano mazuri na watu wetu," alisema Aweso.

Alisema wakati mwingine mtu anapata tatizo la maji na kupiga simu kwenye mamlaka kwamba kuna tatizo ili wasaidiwe, watumishi wanajibu hawana usafiri na kuagiza tabia hiyo ikome.

"Nimeaminiwa kuwa Waziri wa Maji, lazima tuaminike. Haina maana kwamba nitafanya kazi mwenyewe au nina akili zilizopitiliza kuliko wengine. Sekta ya maji ina matatizo mengi na inahudumia uhai wa watu. Tukienda ndivyo sivyo tunapoteza uhai wa Watanzania, sipo tayari kupoteza uhai wa Watanzania," alisema.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Geofrey Mwambe (wapili kushoto), akisalimiana na Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Masasi, Shida Chihongaki, alipolakiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo jana, mjini Masasi, katika ofisi za mkuu wa wilaya hiyo. **PICHA: HAMIS NASRI**

# DC atamani kusweka ndani kijiji kizima

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Simon Mayeka, amesema kungekuwa na mahabusu yenye uwezo wa kupokea watu zaidi ya 3,000, angeitumia kuwasweka ndani kwa muda usiojulikana viongozi na wananchi wote wa kijiji cha Kambikatoto.

Alisema angechukua uamuzi huo kwa sababu viongozi na wananchi wa kijiji hicho wamefanya kosa la kugawana na kuuza shamba la kijiji lenye ukubwa wa ekari 11,228 kwa Sh.milioni 26.5.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika jana kijijini hapo, Mayeka alisema amesikitishwa na hatua ya wananchi hao kwa kushirikiana na viongozi wao kuamua kujitwalia shamba hilo kinyume cha utaratibu wa sheria.

Kutokana na kosa hilo, mkuu huyo wa wilaya alitangaza kuwasimamisha kazi Mwenyekiti wa Kijiji, Ofisa Mtendaji wa kijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na wajumbe wote wa halmashauri ya kijiji ili kupisha uchuguzi wa sakata hilo.

Alisema shamba hilo lilitengwa na serikali ya kijiji kwa miaka mingi iliyopita kwa lengo la malisho na mashamba ya kilimo kwa wanakijiji ambao hawana sehemu ya kulima. Mayeka alisema mbaya zaidi shamba hilo lililouzwa kwa Sh. millioni 26.5, kati ya hizo Sh. milioni 11.5 viongozi waligawana kama posho za wajumbe wa vikao mbalimbali.

"Wananchi wa kijiji hiki mmenisikitisha sana, yaani mnanunua shamba kwa bei ndogo, halafu mnawauzia wafugaji kwa bei kubwa, kwahiyo mmegeuza shamba la kijiji kama sehemu ya kujinufaisha huku mkisahau kufanya hivyo mnatengeneza migogoro ya wakulima na wafugaji hapo badaaye, tena mnabahati sana ninyi yaani ningekuwa na sehemu pa kuwahifadhi ninge wasweka ndani wote,"alisema Mayeka.

Baadhi ya wananchi walisema mpango huo wa uuzaji wa shamba hilo umewaathiri kwa namna mbalimbali kwa sababu eneo moja wanauziwa watu zaidi ya mmoja na imeleta mgogoro miongoni mwao.

"Mkuu wa Wilaya tunakushukuru sana kufika hapa leo, hili suala hata sisi linetuumiza sana, viongozi wetu wametugonganisha mno kwa hili, kwani wanatuuzia eneo moja zaidi ya watu watatu na kusababisha mgogoro" alisema Salum Mjuni.

Aidha, aliwataka wananchi ambao wamejenga au kuanzisha mashamba kwenye mapito ya wanyama (shoroba), kuanza kupisha maeneo hayo haraka kabla sheria haijaanza kuchukua mkondo wake.

Kambikatoto na Sipa vilivyoko tarafa ya Kipembawe ni miongoni mwa vijiji vilivyojengwa kwenye mapito ya wanyama kutoka hifadhi za Taifa za Katavi na Ruaha, na hivyo kufanya wanyama hao kama vile Tembo na Simba kuleta madhara kwa wananchi wa eneo hilo.

## Wizara yaanza kudhibiti ununuzi ofisi za ubalozi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imeanza kudhibiti ubadhirifu wa ununuzi unaoweza kutokea hususani kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo katika balozi.

Hatua hiyo imekuja baada ya serikali kuiongezea fedha wizara hiyo kwenye bajeti ya maendeleo kutoka Sh. bilioni nne mwaka 2019/20 hadi Sh. bilioni 20 kwa mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la asilimia 400.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alisema hayo wakati akifungua mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na maboresho yake ya mwaka 2016, kwa wakurugenzi wa idara na wakuu wa vitengo. Katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Alex Mfungo, alisema uamuzi wa kudhibiti changamoto hizo za ununuzi ni kutokana na asilimia 75 ya fedha za wizara hutumika kupitia ununuzi, hivyo hatua hiyo itasaidia kuokoa fedha za serikali.

"Tunaishukuru sana serikali na bunge kwa kutupatia fedha hizo, hivyo tumeamua kujipanga kwa ajili ya kuhakikisha manunuzi (ununuzi) yanayofanyika (unaofanyika) yanazingatia (unazingatia) umakini wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha tija katika kuitumia ipasavyo fedha hiyo walipa kodi wa Tanzania," alisema.

Sababu nyingine, alisema ni pamoja na kuepuka hoja za ukaguzi zisizo za lazima na kutekeleza majukumu ya serikali yaliyopangwa ili kuleta tija iliyokusudiwa katika kuleta matokeo chanya.

Mhasibu Mkuu wa Wizara hiyo, Swalehe Chondoma, alisema mafunzo hayo yatawasaidia watendaji wake kufahamu namna ya kuanza utaratibu mzima wa kufanya ununuzi.

Alisema mafunzo hayo yatamwezesha kila mtu anayehusika katika mchakato kufahamu wajibu wake katika kutoa huduma bora kwa kuzingatia taratibu na kanuni zilizowekwa.

# Corona ilivyobadili maisha ya wanywaji pombe za kienyeji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



Wanywaji wa pombe za kienyeji wakiwa kilabuni. Ugonjwa wa virusi vya corona ulibadilisha tabia za wanywaji hivyo kulinda afya zao. **PICHA: MAKTABA.**

KANGARA, choya, komoni na wanzuki ni pombe maarufu za kienyeji zinazotengenezwa mkoani wa Dodoma, ambazo unywaji wake ni wa ushirikiano kwa kupokezana chombo cha kunywea kwa watu zaidi ya wawili.

Baadhi ya pombe hizi hutengenezwa kwa kutumia mtama, ulezi, uwele na mahindi na huuzwa kwa bei rahisi ikilinganishwa na bia au kinywaji kingine cha kiwandani.

Kutokana na hali hiyo, uwapo wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu, inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19), umebadili maisha yao kwa kuwa wanalazimika kunywa kila mtu na kikombe chake.

Mwandishi wa ripoti hii alitembelea vijiji vya Bahi Sokoni, Nkome, Mpalanga na Chidilo katika wilaya ya Bahi na baadhi ya maeneo ya Jiji la Dodoma na kushuhudia watumiaji wa pombe hizo kila mmoja akinywa kwenye chombo chake, hali ambayo imeongeza usalama kwa afya zao.

Mbali na kunywa kwenye vyombo vyao, pia wauzaji wa pombe wamebuni utaratibu wa kuwa na vidumu vya kuanzia lita moja hadi tano ambavyo hutumika kujaza na kuuza kulingana na uhitaji wa mteja ambapo lita moja ya pombe hiyo ni Sh. 500.

**WATUMIAJI WANENA**

Fabiana Mazengo anasema corona imesaidia pombe hizo kunyweka kwa ustaarabu ili kuepuka kupata maambukizi ya corona na magonjwa mengine.

"Pombe hizi za kienyeji raha yake ni kupokezana chombo kimoja tukiwa kundi, ili iishe haraka na kuwekewa tena, sasa baada ya huu ugonjwa kuwapo tumebadili muundo wa maisha kwa kiasi kikubwa kwanza unanunua lita mbili ambazo ukinywa peke yako unatosheka na kuendelea na majukumu mengine," anasema.

Maziengo anasema wakati wa corona, wanywaji wa pombe hizo walikuwa wachache kwa hofu ya kuambukizana.

"Hii hofu ilipunguza idadi ya watu kunywa maana tulibandikiwa masharti ya wataalam wa afya ambayo yalitulazimu wengine kununua kwenda kunywa nyumbani, jambo ambalo mtu anaona hapati raha kwa kuwa amezoea kunywa kwa pamoja na wenzake," anasema.

"Sisi tulikuwa tumezoea kupokezana kitochi huku tukikaa pamoja bila hofu ulipokuwa ugonjwa huo tu, tukawekewa masharti kwanza ya kunawa mlangoni, hakuna kusogeleana na kutumia chombo kimoja, kwa kweli ilikuwa tabu," anaongeza.

Naye Mkazi wa Mpalanga, Job Mdolosi, anasema wauzaji huwa na vikombe ambavyo huhifadhiwa kwenye ndoo ya maji safi kwa ajili ya kuosha na kuhudumia watu.

"Wakati wa kunywa ni kila mtu na kikombe chake, hatuchangii tena chombo maisha yetu yameendelea kuwa hivyo wakati wa Corona na baada ya Corona," anasema.

Maria Mcheela, anabainisha kuwa utaratibu unaotumika ni kupewa pombe kidogo kwenye kikombe kwa ajili ya kuonja na baada ya kuipenda ndipo muuzaji anaweka kwenye chombo kulingana na uhitaji wa mteja.

Kefa Jeremia kwa upande wake amezingatia maelekezo ya wataalam kwa kutumia kikombe chake na kunawa na maji safi na sabuni.

"Kwetu hatujawahi kupata matukio mengi ya ukatili kwasababu ya pombe,"anasema.

**WAUZAJI POMBE**

Muuzaji wa pombe za kienyeji Bihawana, Mariam Sijila, anasema wameongeza kwa kiasi kikubwa usafi ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona kwa wanaotumia pombe hizo.

Anasema wakati wa mlipuko wa virusi vya corona hakuna mnywaji mlevi wa pombe ya kienyeji ambaye alikuwa hautambui ugonjwa huo, kutokana na kila moja kuchukua tahadhari zilizokuwa zimetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto . "Mimi kwenye kilabu changu kila mlevi aliyekuwa akiingia humu ndani sharti la kwanza lazima anawe maji ambayo nilikuwa nimeweka hapo mlangoni, pia akiingia humu ndani alikuwa akikutana na tangazo lililokuwa limeandikwa tahadhari zinazotakiwa kuchukuliwa kwa ajili ya kujilinda na ugonjwa huo,"anasema.

Naye, Mandeje Samsoni Muuzaji wa pombe hizo kijiji cha Chidilo, anasema vyombo vinavyotumika vinachemshiwa maji ya moto ili kuua vijidudu.

**MTAALAM WA AFYA AFUNGUKA**

Mratibu wa matibabu na njia za kuzuia maambukizo magonjwa ya mlipuko kutoka Kitengo cha Dharura na Maafa, Wizara ya Afya, Dk. Alex Sanga, anasema ugonjwa wa corona unaambukizwa kwa njia ya maji maji, hivyo kutochangia pombe itasaidia kuepuka baadhi ya magonjwa.

"Majimaji haya aidha ni kutoka njia ya hewa ikiwemo mdomoni, ndio maana tunashauri aidha kama ni chombo cha chakula au cha kunywa, atumie chombo chake inasaidia kuepusha na magonjwa mengine," anasema.

"Afya zinaweza kutofautiana mwingine akawa na midomo imepasuka au vidonda anatokwa damu, inaweza kusababisha maambukizo pia ya magonjwa mengine," anaongeza.

Anafafanua kuwa ni vizuri kila mtu kutumia chombo chake na si kwa wanaokunywa bali hata kwenye jamii kwenye masuala ya vyakula.

"Hii ni njia moja wapo ya kupunguza maambukizo kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine, magonjwa ya mlipuko kwa mfano Corona lakini pia kuna magonjwa mengine yanaambukizwa kwa maji maji,"anasema na kuongesha:

"Utafiti unaonesha uwezekano ni mdogo lakini upo na umetokea, kwa mfano kama mtu amepasuka mdomo unatoa damu akatumia chombo hicho hicho kunywa pombe na kumpa mwenzake anaweza kupata magonjwa kama vile Ukimwi."

Aidha, anasema Wizara ilitoa elimu na miongozo mbalimbali ya kuzuia maambukizo ya Corona kwa watanzania ikiwemo watumiaji wa pombe hizo.

**MIONGOZO ILIVYOTOLEWA**

Ofisa Afya Mwandamizi kutoka Wizara ya Afya, Innocent Swai, alisema Wizara hiyo ilitoa miongozo kwenye Halmashauri namna ya kukabiliana na ugonjwa huo kwenye maeneo yao ikiwemo vilabu vya pombe na minada.

"Tulitoa mwongozo wa namna ya kuzingatia kukaa kwa umbali kwenye maeneo yote yenye mikusanyiko, kama ukienda hospitali utakuta kuna alama hapa kaa hapa usikae,"anasema.

Anaeleza pia kuna miongozo ya watu kutofanya mikusanyiko isiyo ya lazima na kututumia vifaa jumuishi ikiwamo vyombo vya kunywea pombe.

"Pia mahali kwenye mikusanyiko kuwe na vifaa vya kunawia mikono, tulitoa matangazo ya namna Corona inavyoambukizwa na namna ya kujikinga, ufanye nini ukiwa na dalili,"anasema.

**UTAFITI WA POMBE**

Utafiti uliofanywa nchini na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2010, ulionyesha asilimia 87 ya Watanzania wanakunywa pombe za kienyeji huku miji ya Dar es Salaam na Moshi ikitajwa kuwa inaongoza kwa kuwa na watumiaji wengi wa pombe hizo.

Hata hivyo, idadi hiyo imetajwa na WHO kuchangia kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii.

**Habari hii imeandikwa kwa ufadhili wa Women Writers Forum (WRIFOM)**

## Serikali yazindua mifumo udhibiti wa matumizi hewa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeanzisha mifumo miwili ya kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima, kuhakikisha taarifa zinapatikana kwa wakati na kwa ufasaha.

Mifumo hiyo ni Usimamizi wa Taarifa za Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Umma na Wakala wa Serikali, pamoja na Mfumo wa Uchambuzi wa Taarifa za Fedha. Akizungumza katika uzinduzi wa mifumo hiyo, Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, alisema kuwa mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wajumbe wa Bodi za Yaasisi za Umma na Wakala wa Serikali umejengwa na watalaam wa ndani.

Lengo kuu, kwa mujibu wa Mbuttuka ni kuhifadhi taarifa za uteuzi wa wajumbe hao wa bodi, wasifu wao, idadi ya taasisi wanazohudumu, aina za wajumbe wao pamoja na kurahisisha utolewaji wa taarifa wa wakati.

Alisema kuwa mfumo huo utasaidia ofisi ya Msajili wa Hazina na mamlaka za uteuzi kupata taarifa mapema kuhusu bodi kumaliza muda wake, wajumbe wa bodi wanaodumu katika bodi kwa zaidi ya miaka mitatu, upatikanaji kwa bodi kwa wakati pale inapomaliza muda wake. Mbuttuka alisema kuwa uwapo wa mfumo huo mpya utaondoa tatizo la muda mrefu la baadhi ya wajumbe wa bodi kuteuliwa katika bodi ya tatu, watendaji wakuu kukaimu muda mrefu na kuzifanya mamlaka za uteuzi kupata taarifa kwa wakati kuhusu hali za bodi katika taasisi za umma.

Kuhusu Mfumo wa Uchambuzi wa Taarifa za Fedha, Mbuttuka alisema utakuwa wa kieletroniki.

Akizindua mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa taarifa za wajumbe wa bodi, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema ofisi ya Msajili wa Hazima imekuwa kwa muda mrefu na tatizo la kuzikumbusha mamlaka za uteuzi kuhusu kumalizika kwa bodi hizo, hivyo kuwapo kwa mfumo huo utakuwa kitendea kazi muhimu.

Dk. Ndumbaro alisema kulikuwa na taasisi nyingi ambazo hazipati bodi hizo kwa wakati, hivyo kupitia mfumo huo bodi zitapatikana kwa wakati kwa lengo la kusaidia serikali kufikia malengo yake ikiwamo kudhibiti hujuma.

# TAMWA yataka jamii kuanika matukio ya ukatili wa kijinsia

**Na Jenifer Gilla**

JAMII inasisitizwa kuibua na kufichua matukio yote ya ukatili wa kijinsia yanayoendelea kuanzia ngazi familia na katika taasisi kama vile shuleni, vyuoni na sehemu ya kazi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, katika Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Duniani.

Katika mkutano huo uliobebwa na kaulimbiu 'Pinga ukatili wa kijisia, mabadiliko yanaanza na wewe' Reuben alisema TAMWA imebaini kuwa licha ya vyombo vya dola kuchukua hatua bado kuna matukio ya ubakaji, ulawiti, mimba za mapema na udhalilishaji.

"Tukiyakalia kimya matukio haya hatuwezi kupata suluhisho. Ni muhimu kuripoti bila kuona haya ili vyombo vya dola vichukue hatua," alisema Reuben.

Aliyataja baadhi ya matukio ya ukatili yaliyotokea mwaka huu yaliyoripotiwa na utafiti uliofanywa na vyuo vikuu vya Dodoma na Mlimani kuwa ni la Mwenyekiti wa Kijiji cha Ijinga, wilayani Magu , Badri Masengo (40), kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la sita mwenye miaka 15.

Pia tukio la kubakwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi ya Montfort (10) na mwalimu wake Anserson Eneser, lililotokea Novemba 11, mwaka huu.

Hali kadhalika huko visiwani Zanzibar, Haroub Abdallah Had, alidaiwa kumbaka mtoto wa miaka mitano October 10, mwaka huu, wilayani Wete, Pemba.

"Utafiti huo uliochapishwa hivi karibuni, uliofanywa katika vyuo vikuu vya Mlimani na Dodoma ni angalizo tosha kuwa ukatili wa kijinsia upo wa aina nyingi, katika mazingira tofauti, kwa jinsia zote na katika sekta mbalimbali binafsi na za umma" alisema Reuben

Maadhimisho hayo mwaka huu yalifanywa na TAMWA na Kituo cha Usuluhishi (CRC) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Marekani nchini.

Akizungumza katika maadhibisho hayo, Ofisa wa Siasa kutoka Ubalozi wa Marekani, Dk.Willow Williamson, alisema kuwa Ubalozi wa Marekani unatambua umuhimu wa mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ni nafasi kwetu sote kupaza sauti juu ya ukatili wa kimwili, kisaikolojia na kihisia wanaopitia wanawake duniani" alisema Willamson.

Aliongeza kuwa mwanamke mmoja kati ya watatu anapitia ukatili wa kimwili au kingono duniani na hufanyiwa zaidi na wenzi wao, 71% ya wanawake hupitia biashara ya binadamu na wasichana watatu kati ya wanne wananyanyasika kingono.

Naye Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi (CRC), Chadness Munuo, alisema kuwa kuna kiwango cha juu cha masuala ya ukatili na wanapokea kesi nyingi za kusuluhisha migogoro ya kifamilia kwa mwaka mojawapo ikiwa ukatili wa kijinsia.

Aliongezea kuwa, kwa miaka 16 sasa wamehifadhi kesi walizosuluhisha 25 ambazo wahusika wamekubali zihifadhiwe, lakini zipo nyingi ambazo wahusika wamekataa zisihifadhiwe.

Katika maadhimisho hayo pia kuliongelewa umuhimu wa wanaume kushirikishwa katika masuala ya ukatili wa kijinsia ili wawe chachu ya kuleta mabadiliko katika janga hilo.

Mwakilishi kutoka Mtandao wa Ushiriki wa Wanaume katika Ukatili wa Kijisia (MET), Marcella Lungu, alisema wanaume wanaweza kushiriki kutokomeza utatili wa kijinsia hivyo wasiachwe nyuma.



Baadhi ya wahitimu wa Shahada ya Uuguzi katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), wakila kiapo cha utii wakati wa mahafali yaliyofanyika jana, chuoni hapo jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Kairuki yafadhili masoko ya juu wafanyakazi

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), kimeendelea na mpango wake wa kufadhili masomo ya wafanyakazi wake kwa ngazi ya uzamili na uzamivu ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Charles Mgone wakati wa mahafali ya 18 ya chuo hicho yaliyofanyika chuoni hapo, Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Katika mahafali hayo, wahitimu 146 walitunukiwa stashahada ya uuguzi, 53 shahada ya uuguzi, 183 shahada ya udaktari wa binadamu na wawili shahada ya uzamivu ya udaktari wa binadamu.

Alisema wahadhiri wanne wamemaliza mafunzo yao ya uzamili hivi karibuni akiwataja wanufaika hao kuwa ni Dk. Fulgence Mpenda, Dk. Jane Nyandele, Dk. Hosiana Msechu na Dk. Zahra Moraweji.

Prof. Mgone alisema kwa sasa chuo hicho kina wahadhiri 15 wanaosomea shahada ya uzamivu na saba shahada ya uzamili katika fani mbalimbali huku wahadhiri sita wakipandishwa vyeo katika fani mbalimbali.

Alisema katika kuboresha ufundishaji chuo kimeajiri wafanyakazi wapya ili kuendana na ongezeko la wanafunzi na tangu Desemba 2019 mpaka Novemba mwaka huu chuo kimeajiri wafanyakazi wapya wanane.

Kuhusu utafiti, Prof. Mgone alisema tafiti mbalimbali zinaendelea kufanywa na wanataaluma wa chuo na wanafunzi wake wa ngazi zote zingine zikihusu magonjwa ya kuambukizwa na yale yasiyo ya kuambukiza.

Alisema kwa mwaka 2020 baadhi ya wataalam wa chuo hicho wametoa machapisho kadhaa katika majarida ya kisayansi yakiwamo ya uchambuzi yakinifu kuhusu elimu ya uuguzi na ukunga nchini na utafiti kuhusu njia mpya za kutibu maralia.

Makamu mkuu huyo alitaja machapisho mengine kuwa ni kuhusu uhusiano kati ya ugonjwa wa seli mundu na malaria, dalili za mwanzo za kuelekea kupata ugonjwa wa kisukari na aina ya magonjwa yanayowasibu watoto wachanga waliozaliwa kabla ya wakati.

"Kwa niaba ya chuo napenda kuwapongeza wanataaluma na wanafunzi wote kwa hayo machapisho ambayo yametambulika kitaifa na kimataifa," alisema

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Afya na Elimu la Kairuki, Kokushubila Kairuki, aliwapongeza wafanyakazi wote wa chuo hicho kwa namna wanavyozidi kukipandisha hadhi mwaka hadi mwaka kutokana na kila mmoja kuwajibika kwa upande wake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaume pia wapaze sauti kuhusu ukatili wa kijinsia

**WIKI** hii Tanzania kupitia wadau mbalimbali, iliadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, ikiwa nia ya kupaza sauti ya kupambana na hatimaye kutokomeza vitendo hivyo ambavyo vimezidi kushika kasi nchini.

Katika maadhimisho hayo ambayo yaliambatana na shuhuda na makongamano mbalimbali, wadau kutoka kila kona waliweka wazi sababu kadhaa zinazofanya kushamiri kwa vitendo hivyo.

Moja ya mikutano kuhusu maadhimisho hayo, ulifanyika Zanzibar na kushirikisha wadau mbalimbali liliwamo Jeshi la Polisi. Katika mkutano huo, Meneja wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliweka bayana sababu za vitendo hivyo kuzidi kushamiri katika jamii.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kuendelea kwa vitendo hivyo kuota mizizi ni baadhi ya wazazi na walezi kumalizana na wahusika, hususan wanaowapa ujauzito wanafunzi, nje ya mahakama kwa kupokea fedha au zawadi. Alisema wakati mwingine wahusika wanakuwa hawafiki mahakamani pindi kesi zinapofunguliwa na kuanza kusikilizwa, hatua ambayo inasababisha kukosekana kwa ushahidi na hatimaye kufutwa.

Licha ya Dk. Mzuri kueleza hayo, taarifa mbalimbali zilizotolewa katika makongamano mbalimbali wakati wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, zilieleza kuwa rushwa na kupoteza ushahidi ni vyanzo vikuu vya ukatili wa kijinsia kushika kasi katika jamii.

Jambo lingine lililobainishwa wakati wa mikutano hiyo ni kwamba baadhi ya watu wanaofanyiwa vitendo hivyo, wengi wakiwa wanawake na wasichana, hukaa kimya bila kufikisha mambo hayo kwenye vyombo vya sheria kwa kuhofia kuachika au kupata aibu kwa jamii.

Hayo ni mambo yaliyozoeleka ndani ya jamii kwani kila mwaka hadithi kama hizo zimekuwa zilisimuliwa kwenye mikutano na maadhimisho kama hayo. Lakini kubwa zaidi lililoibuka ni juu ya vipigo vya wanawake kutoka kwa wake au wapenzi wao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, alisema wanaume wamekuwa wakifanyiwa ukatili na wake zao, vikiwamo vipigo lakini wamekuwa hawaripoti mambo hayo ili hatua zichukuliwe.

Kiongozi huyo wa serikali alisema sababu kubwa inayochangia wanaume kushindwa kupaza sauti juu ya ukatili wanaofanyiwa na wenzi wao au marafiki kuogopa aibu na kuchekwa mbele ya jamii. Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba mazoea yaliyoko ndani ya jamii ni wanaofanya vitendo hivyo ni wanaume dhidi ya wanawake.

Miaka ya 2000, mwandishi wa habari wa shirika la Utangazaji Tanzania, Mwadawa Lugongo, katika utafiti wake ambao uliibua gumzo katika jamii, alisema zaidi ya asilimia 30 ya wanaume waliohojiwa walikiri kupata vipigo kutoka kwa wake zao, hivyo kuonyesha kwamba kuna vitendo kama hivyo ndani ya jamii.


Kuibuliwa kwa hoja hizo, kunatoa mwanga kwamba tofauti na ilivyozoeleka awali kwamba ni wanawake tu ndio wanaofanyiwa vitendo hivyo, mtazamo wa harakati za kupinga ukatili wa kijisia uchukue sura mpya kwamba jinsia zote mbili ni waathirika wa suala hilo.

Wanaume nao, kwa mantiki hiyo, wanapaswa kupaza sauti zao kutokana na kunyanyaswa na wanawake, si kwa kupita vipigo tu hata kwa kukimbiwa na kupokwa mali walizochuma na wanaume kunapotokea tatizo lolote kama vile mwanamume kukosa kazi au kuyumba kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Matumizi kiasi ya chumvi yanaepusha ugonjwa huu

**Na Sabato Kasika**

**SHINIKIZO** la damu linaelezwa na wataalam wa afya kuwa ni msukumo wa damu kwenye kuta za mishipa inayosafirisha damu na hupimwa kwa kutumia mkanda wa mpira unaovalishwa mkononi na kujazwa hewa.

Inaelezwa kuwa sababu za watu wengi kupata tatizo hilo la shinikizo la damu la juu huwa hazijulikani lakini kuna baadhi ya mambo ambayo huchangia kwa mtu kupanda kupita kiasi.

Miongoni mwa mambo hayo ni umri mkubwa wa zaidi ya miaka 65 kwamba wenye umri huo huwa na presha ya juu kuliko vijana na watoto, unene wa kupitiliza, kuwa na ndugu wa damu wenye tatizo la presha.

Aidha, mengine ni mazoea ya kutumia chumvi nyingi kwenye vyakula, ulevi wa kupindukia na kutopata usingizi wa kutosha na mengine yanayofanana na hayo.

Pamoja na hayo yote, ninataka kujikita zaidi kwenye matumizi ya chumvi, ambayo daktari bingwa wa magonjwa ya binadamu, Dk. Lucas Nzobendo, anashauri yapunguzwe.

Daktari bingwa huyo kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, anasema chumvi ni madini yenye umuhimu na faida nyingi na katika maisha ya kawaida ni vigumu kukosa madini hayo au kiungo hicho kwenye familia mbalimbali.

Kiungo hicho hutumika jikoni kwa ajili ya kuongeza ladha kwenye chakula na pia hutumika kuhifadhi vyakula na kuoka. Pamoja na matumizi hayo chumvi ina madhara kiafya iwapo mtumiaji ataunga kwenye chakula kiasi kisichotakiwa.

Mtaalam huyo wa afya anashauri watu kuwa makini na matumizi makubwa ya chumvi na kwamba watu wenye umri mkubwa wanahitaji chini ya gramu moja (kijiko kidogo cha chai) kwa siku.

Wakati watu wa umri huo wakitumia kiasi hicho, watoto wanahitaji kidogo zaidi, huku watu wenye umri wa kati wakitakiwa kutumia chumvi gramu sita kwa siku ili kuwa salama zaidi dhidi ya tatizo hilo.

Hata hivyo, anasema watu wengi wanakula chumvi zaidi ya gramu nane kwa siku, hali ambayo inawaweka katika hatari kiafya. Kutokana na hali hiyo, anasema wanatakiwa kubadilika na kufuata ushauri wa wataalam wa afya.

Ni wazi kwamba kupunguza ulaji wa chumvi kunaweza pia kupunguza shinikizo la damu na hatari ya magonjwa mengine, huku akishauri kushuka hadi kutoka gramu sita hadi kufikia tatu kwa siku.

Hiyo inatokana na kile ambacho mtaalam huyo anasema, iwapo watu wenye umri wa kawaida wakipunguza matumizi ya chumvi hadi kufikia gramu tatu kwa siku, watakuwa wamejiweka katika nafasi nzuri ya kiafya.

Shinikizo la damu linaelezwa kuwa ni moja ya sababu kubwa za kiharusi na matumizi ya chumvi nyingi yanatajwa kuchangia shinikizo hilo, hivyo chumvi ni sababu kubwa ya ugonjwa huo.

Aidha, kiharusi ni mojawapo ya magonjwa yanayokuja na umri mkubwa, lakini kinaweza kuepukika kwa kuzuia shinikizo la damu kwa njia ya kupunguza ulaji chumvi, mazoezi na kula vyakula vya kuleta afya njema.

Ikumbukwe kuwa kiharusi kimewahi kutajwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa ni muuaji namba mbili duniani kati ya magonjwa yote yanayosababisha vifo vingi duniani.

Kwa hali kama hiyo, ni vyema vyanzo maradhi, ambavyo viko ndani ya uwezo wa kila mmoja wetu, kuchukua hatua zinazotakiwa ikiwamo kutumia chumvi kwa kiasi kinachotakiwa.

Si hayo tu bali inaelezwa kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ulaji wa chumvi kwa wingi na saratani ya tumbo, hali ya mifupa kuwa rahisi kufunjika, kutokana na upungufu wa kalsiamu na vitamini D.

Inaelezwa kuwa iwapo presha ya damu ni kubwa, ina maana mishipa ya damu na moyo vipo katika shinikizo kubwa, na likiendelea huweza kusababisha moyo kushindwa kufanya kazi.

Vilevile kusababisha moyo kutanuka, shambulio la moyo, kiharusi, kuharibu figo hivyo kushindwa kufanya kazi, kusababisha upofu na wakati mwingine mtu kufariki dunia.

Njia sahihi ni kila mmoja kuchukua hatua za kuepuka yale yote yanayoweza kusababisha ugonjwa huo, hasa kupunguza matumizi ya chumvi na mengine yanayokatazwa na wataalam wa afya.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Dawa ya rushwa ya ngono vyuo vikuu hii hapa

GAZETI hili la Novemba 28, 2020 lilitoa ripoti ya utafiti juu ya kutamalaki kwa rushwa ya ngono kwenye taasisi za elimu ya juu. Utafiti huu ulivitaja vyuo vikuu viwili vya umma kimoja kikongwe na kingine kikubwa nchini. Kama kweli hali iko hivi, kwanza hii ni aibu. Na pili ni kielelezo kuwa mfumo wetu wa elimu una matatizo yanayopaswa kushughulikiwa bila huruma kama ilivyokuwa kwenye kadhia ya vyeti vya kughushi na ajira na wanafunzi hewa. Tatu, udhaifu na uozo huu utumike kama fursa ya kurekebisha mfumo mzima ili uweze kuwa wajibikaji na kuzaa matunda tarajiwa.

Leo, tutatoa baadhi ya mapendekezo ya kupambana na kuondoa aibu na kadhia hii kama ifuatavyo:

Mosi, tujenge mfumo wenye uwazi katika uendeshaji taasisi zetu na utendaji kazi ambapo lazima kuanzishwe mfumo wa utathmini wa walimu na wanafunzi sawia na sambamba. Hapa ni kwamba, walimu wawatathmini wanafunzi na wanafunzi wawatathmini walimu wao. Hapa Kanada, mwalimu anamfanyia mwanafunzi tathmini na kadhalika, kila baada ya kumaliza somo wanafunzi hupewa fomu za kuwatathmini walimu wao bila kuweka majina yao. Utaratibu, licha ya kuleta uwajibikaji na ushindani, unajenga imani kwa wanafunzi na walimu. Hapa hakuna kuchezeana wala kupunjana. Ukisoma unasoma kweli kweli vinginevyo, utatafuta la kufanya kama hufai.

Pili, tuanzishe utaratibu wa walimu kuwajibika kisheria kuwa na sera ya mlango wazi ambapo kila kinachofanyika ofisini kinaonekana. Hili husaidia si kuleta uwazi tu bali hata kuheshimiana na kuwajibika.

Tatu, Tume ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ihakikishe inaweka mashushushu wake vyuoni kwenye ngazi zote kuanzia wanafunzi hata wafanyakazi na uongozi. Hili, licha ya kubaini tatizo na kulishughulikia vilivyo mapema, litajenga hofu na mazingira ya uwazi na uwajibikaji si kwa walimu tu bali hata wanafunzi wanaotaka kupata shahada za dezo bila kustahiki au kuzihenyekea.

Nne, wasomi wajiepushe na kujichafua na kuwaharibia maisha wanafunzi. Msomi aliyeelimika vilivyo anapaswa kujua mipaka yake. Kutumia elimu au mamlaka kujipatia rushwa ya aina yoyote ni ushahidi tosha kuwa mhusika licha ya kutokuwa muadilifu hajaelimika ipasavyo na vilivyo. Watu wa namna hii wanapaswa ima kufukuzwa kazi au kurejeshwa darasani ili wasome na kuelimika.

Tano, wale wanaopatikana na hatia wapewe adhabu kali ili liwe somo kwa wengine wanaotarajia kujihushisha na jinai na uchafu huu. Hapa lazima adhabu iwe kwa wote, yaani mtoa na mpokea rushwa. Wanafunzi wanaoruhusu kuchezewa wanakuwa washirika wazuri. Kwanini wasiripoti kadhia hii ili kuanzisha mgogoro ambao mamlaka zitaushughulikia ili kuepuka kupatilizwa au kuonewa? Maana bila kufanya hivi, wanafunzi watakaoripoti uchafu huu, wanaweza kuonewa ima na wale waliowatuhumu au marafiki na washirika wao. Lazima kuwepo na namna ya kuwalinda wanafunzi watakaotoa malalamiko ya kuombwa rushwa. Pia hapa lazima tuwe makini wasitokee wanafunzi wakatumia fursa hii kuwakomoa wabaya wao ambao ni walimu wao. Ifikie mahali hata mwanafunzi akipendekeza kutoa rushwa ya ngono kwa profesa, mhusika naye amripoti ili kutenda haki kwa wote. Maana rushwa mara nyingi, ni makubaliano baina ya mtoaji na mpokeaji.

Sita, wanafunzi nao waache njia za mkato. Mfano, hapa Kanada, hakuna namna ya kupata shahada bila kuihangaikia. Mfano, shahada za kwanza, humjengea mwanafunzi uwezo wa kujitafutia maarifa huku za uzamivu zikimpa changamoto ya kuweka maarifa yake kwenye vitendo huku za uzamili zikimpa changamoto mwanafunzi kuyazalisha na kuyatumia maarifa na ujuzi wake. Huwa nashangaa kuona maprofesa au madaktari ambao licha kuficha tasnifu zao, hawachapishi. Huwezi kuwa mwanataaluma aliyeiva kweli kweli ukashindwa kuchapisha. Usipofanya hivyo, unahatarisha ajira yako. Kwani kazi ya profesa siyo kufundisha tu bali kuzalisha elimu mpya kwa njia ya utafiti na machapisho. Hii humsaidia mhusika na taasisi yake kutoa mchango kwa jamii yake kitaaluma.

Saba, kuna umuhimu wa kuanzisha elimu ya kupambana na rushwa kwa jamii ili wahusika wajue madhara yatokanayo na maamuzi ya kuomba au kutoa rushwa. Kama ilivyo kwa magonjwa ya kutisha, rushwa ichukuliwe kama janga ambalo dawa yake ya kwanza iwe ni kuielimisha jamii juu ya madhara yake na yatokanayo na kujihusisha nayo.

Nane, tujenge mfumo wa kushukiana na kutoaminiana. Hapa Kanada, kwa mfano, hakuna cha kuaminiana kienyeji. Kila mtu anajua haki zake; anajua mipaka ya mamlaka na haki zake. Ukijenga jamii ya namna hii, licha ya kutenda haki, unakuwa na jamii makini na yenye ushindani na kuheshimiana. Jamii ya namna hii lazima itaendelea. Hii ni kwa sababu kila anayepewa jukumu, licha ya kujua wajibu wake, anakuwa ameiva kweli kweli kulitekeleza huku akijua madhara ya kulala kwenye usukani kama wasemavyo huku.

Tusiangalie rushwa ya ngono tu. Tuangazie na rushwa nyingine ambazo huwafanya watu wasiostahiki kuwa na ukwasi usiokuwa na maelezo ya kueleweka. Mfano, hapa Kanada, huwezi kulala maskini ukaamka tajiri kama ilivyokuwa nyumbani. Kila mtu hujaza taarifa zake za mapato kila mwaka. Hivyo, kipato cha kila mtu kinajulikana na hivyo ndivyo anavyopaswa kuishi. Hakuna njia za mkato au mission town kama nyumbani ambako mtu anaweza kulala maskini akaamka tajiri bila vyombo vya sheria kumshika, kumhoji, kumtaka maelezo na kumchukulia hatua pale anapogundulika kuwa na kipato kisichoweza kutolewa maelezo. Utaratibu huu huondoa mazingira na motisha wa wananchi kujiingiza kwenye jinai ya aina yoyote kama njia ya kujiongezea kipato.

Tumalizie kwa kuhimiza kuwa lazima tufanyie mfumo wetu wa elimu pamoja na mingine maboresho na marekebisho makubwa ili kuweza kupata matokeo tarajiwa.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Si lazima sherehe hotuba zinatosha

MIONGONI mwa mambo yaliyoishitua nchi baada ya Rais John Magufuli kuingia madarakani mwaka 2015, ni kuamua kufuta shamrashamra za baadhi ya sherehe na fedha zilizokuwa zitumike, kuhamishiwa kwenye shughuli za maendeleo.

Ilishazoeleka kuwa kila mwaka lazima Watanzania washerehekee kumbukizi za matukio mbalimbali yaendanayo na historia ya nchi, ikiwa ni pamoja na sherehe za Uhuru, uliopatikana mwaka 1961 kutoka kwa Wakoloni.

Walishazoeshwa kuwa siku muhimu sana kwa historia na mustakabali wa Taifa ambapo inasemekana fedha nyingi zilitumika katika sherehe hizo, kwa ajili ya maandalizi ya siku zenyewe, lakini pia gharama mbalimbali za safari, mabango na posho kwa viongozi na washiriki wengine.

Fedha hizo zilijenga miundombinu ya barabara, hospitali, nakadhalika. Ni kweli kilichofanywa na fedha hizo kinaonekana na hakuna ubishi, kwamba yawezekana fedha nyingi zilikuwa zinaishia mifukoni mwa wajanja, tukifurahia Uhuru bila maendeleo.

Ni jambo la kupongeza hasa kwa uamuzi mgumu kama huo, ambapo pia mara moja mwaka huu tulikosa kuwasha Mwenge wa Uhuru na kuukimbiza hatimaye kuzimwa siku ya kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Oktoba 14 ya kila mwaka. Hiyo ilitokana na kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19.

Lakini je, mbali na manufaa hayo yaliyopatikana kutokana na kuahirishwa au kufutwa kwa shamrashamra, kihistoria Watanzania na hasa watoto wa kizazi cha leo na walioko shuleni wanajifunza nini?

Ni kweli, kwamba shamrashamra hizo zilipoteza fedha za maendeleo, ni kweli pia siku hizo hazikupewa uzito, hasa pale zilipoahirishwa na watu kukaa majumbani bila kwenda kazini na kudai tunakumbuka siku ya Uhuru, nakadhalika.

Yawezekana ikawa kweli pia, kuwa fedha zilitumiwa vibaya, kwa kuwa haiingii akilini mabilioni ya fedha kutumika kufanya magwaride na maandamano, huku ikifahamika kuwa askari wanaofanya magwaride hiyo ni sehemu ya kazi yao na wanalipwa kwa hilo.

Lakini pia watumishi na viongozi wa Serikali hawatakiwi kulipwa ili kwenda kusherehekea kumbukumbu ya Uhuru na kuhutubia wananchi, hata kama kuna wacheza ngoma, isingewezekana walipwe mamilioni ya fedha kuburudisha kwa saa moja au chini ya hapo. Ni ubadhirifu na ukosefu wa uzalendo.

Inawezekana pia uamuzi tulioufanya wa kufuta sherehe, tuliufanya kwa nia njema, lakini tukasahau athari zake kihistoria. Kwamba mbali na kufundishwa shuleni, ni wapi kwingine ambako kizazi kinaweza kujifunza historia, kwa maana ya kupata Uhuru au ni jinsi gani Jamhuri ilipatikana, achilia mbali Muungano wa Tanganyika na Zanzibar?

Kama uamuzi huu utaendelea, kwa lengo hilo hilo la kutumia fedha kwa maendeleo ya nchi, basi ipo haja ya siku hizo kutopita bila kufanyika chochote cha kutukumbusha matukio hayo muhimu ya kihistoria.

Mathalan, Rais ambaye ndiye Mkuu wa Nchi, asiache tu wananchi tukajikalia majumbani tukilewa au kulala, bila kusikia lolote kuhusu siku hizo muhimu, hata kupitia vyombo vya habari, hususan luninga.

Siku hizo Rais ajipange angalau kuhutubia Taifa akielezea umuhimu wa siku hizo au matukio kama hayo, ili wananchi na vizazi vipya, wasipoteze kumbukumbu hizo muhimu na kuonekana kuwa na Taifa lisilo na historia yake.

Ukimya ukiendelea huku siku zikitajwa na kubaki kwenye kalenda, ni rahisi sana Watanzania wa kizazi kijacho, wakakosa hata kumfahamu Mwalimu Nyerere, wakakosa kujua Tanzania ilianzia wapi na ilitokeaje.

Ukimya huo utatufanya tushindwe kuheshimu si tu alama, bali hata tunu tulizoachiwa na waasisi wetu na kuonekana kama Taifa la kuazima na si tulilolijenga wenyewe. Hakuna Taifa duniani lisilosherehekea uhuru wake, siku hizo hujulikana kama Siku ya Taifa. Kifanyike chochote, ilimradi historia isipotee.

Yapo mataifa ambayo yamekuwa hata yakifikia hatua ya kuadhimisha siku za kuzaliwa viongozi wao, sembuse Taifa? Hivyo ni vema viongozi wetu wakaliona hilo, ili hata kama tutakuwa tunaokoa fedha na kuzipeleka kwenye maendeleo, lakini bado historia ya nchi

## KONA YA UKWELI

# Magufuli ana mipango kutafuta uhuru wa kweli, aungwe mkono



Na Thobias Mwanakatwe

MIAKA mitano ya utawala wa Rais John Magufuli na mitano mingine aliyoanza nayo Novemba, mwaka huu, ni wazi kuwa mipango yake ni kuifanya Tanzania kuwa taifa linalojitegemea.

Dalili zinajionyesha wazi kwamba Rais magufuli, maarufu kama JPM, amedhamiria kufanya kweli ndiyo maana kuna miradi mikubwa iliyojengwa na inayoendelea kujengwa ambayo inatekelezwa kwa fedha za ndani bila kutegemea wafadhili.

Kubwa ambalo liliwaacha midomo wazi wafadhili ni pale alipoamua Tanzania kugharamia uchaguzi mkuu kwa mabilioni ya fedha. Hiyo ni kutokana na msimamo wa JPM kutaka Tanzania isimame kwa mikono yake yenyewe ndipo tunaposema uhuru wa kweli wa taifa hili unakuja.

Ninaposema uhuru wa kweli unakuja simaanishi kwamba Tanzania bado hatuna uhuru. Ninachomaanisha ni kwamba unapokuwa tegemezi kwa mtu au nchi fulani, unakosa uhuru wa kujiamulia mambo yako kwa sababu yule aliyekusapoti au kukupiga tafu atataka ufanye mambo anayoyapenda yeye. Huko ndiko kukosa uhuru wa kweli.

Uhuru wa kweli wa taifa lolote unatafsiriwa katika uwezo wa taifa husika kutambua changamoto za watu wake na kuzitafutia majibu bila msaada kutoka nje au kwa jirani. Taifa linapokuwa halina uwezo wa kutatua matatizo yake ya ndani mpaka lipate msaada toka nje, linaitwa tegemezi na kamwe haliwezi kuwa huru..

Aidha, uhuru wa taifa lolote utafsiriwa kwa uwezo wake wa ndani kutatua changamoto zake na kuzitumia fursa zake kupiga hatua za kimaendeleo.

Uwezo wa nchi kiuchumi ni kuzalisha bidhaa na huduma na kuziuza ndani na nje ya mipaka yake. Hii ndiyo ishara ya kwanza ya uhuru wa taifa. Pia uwezo wa nchi husika kuendesha mipango yake na mambo yake ya ndani kwa kutumia mapato yake, ni tafsiri ya nchi kuwa huru.

Uwezo wa kukusanya na kugawanya mapato ya serikali kwenda katika shughuli za maendeleo pia ni kipimo kizuri cha uhuru. Vilevile, uwezo wa nchi husika kupunguza utegemezi wa misaada ya kifedha, kitechnolojia na kielimu, pia ni ishara ya uhuru wa kweli katika Taifa.

Kadhalika, uhuru wa nchi upo katika kudumisha utamaduni wake dhidi ya utamaduni wa kigeni na daima taifa linasimama kutetea tunu zake kama utu, lugha, mavazi, miiko, desturi na utamaduni.

Uhuru wa bendera au wa kisiasa bila uhuru wa kiuchumi ni kazi bure, hivyo taifa linapaswa kuutafuta uhuru wa kiuchumi kwanza kwa gharama yoyote.

Japo kumekuwa na juhudi za makusudi katika awamu zote za uongozi wa taifa la Tanzania katika kutafuta uhuru wa kiuchumi, awamu ya tano imejipambanua kwamba inataka Tanzania kuwa mbia wa maendeleo na si tegemezi wa maendeleo.

Juhudi za wazi za kujitegemea kupitia ukusanyaji wa mapato na ujenzi wa miradi ya kimkakati ni ishara ya kuonyesha taifa linautafuta uhuru wa kweli. Kuna nia ya dhati kabisa kila mtu anaona ya kuutafuta uhuru wa kweli wa kiuchumi, matokeo yameanza kuonekana wazi baada ya nchi kufikia uchumi wa kati.

Mipango ya serikali ya JPM imeanza kuwatisha mabeberu wa ndani na wa nje, hivyo kuwapo kwa vita vya wazi vya kuikwamisha Tanzania kufikia ndoto yake ya kuwa taifa huru kiuchumi.

Kama mipango na hatua zinazochukuliwa na serikali zitafanikiwa, ni hakika Tanzania itakuwa miongoni mwa mataifa yenye uchumi mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, hivyo kuwa na uwezo wa kujiamulia mambo yake.

Kadhalika, uchumi mkubwa utatuwezesha katika uwekezaji katika maeneo ya kimkakati katika maendeleo ya taifa, mfano katika miradi ya sayansi na technolojia kupitia vyuo vyetu vya ndani kwa kuzalisha teknolojia kwa matumizi ya nchi na matumizi ya ndani.

Uchumi mkubwa utatupa uhuru wa kutengeneza ajira na miradi mengine ya kijamii kuweza kuwahudumia wazee na Watanzania kwa ujumla kupitia miradi ya afya, makazi na nyanja zingine za maendeleo yao.

Hatua ambazo zinachukuliwa na serikali ya awamu ya tano zinaonyesha wazi kuwa ina lengo la kufanya mambo makubwa kuwa nchi inayojitegemea na si tegemezi. Shime Watanzania tumuunge mkono JPM.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Thamani ya muda katika kazi na malezi ya familia



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

UMUHIMU wa rasilimali watu mahali pa kazi ni chachu ya mafanikio katika sekta yoyote ile. Kwa maneno mengine, mafanikio yanategemea watu. Ili mafanikio hayo yawe ya kweli, jambo la msingi ni kuwa na wafanyakazi wenye furaha.

Furaha na utendaji kazi kwa ufanisi mahali pa kazi, kimojawapo kinapokosekana basi hakuna tija na ufanisi mahali pa kazi. Kutokana na ukweli huo, waajiri wamekuwa wakiwekeza katika huwajengea uwezo wafanyakazi na watumishi wao na kujitahidi kuhakikisha wana furaha siku zote.

Zaidi ya hayo, ili mfanyakazi afanye kazi kwa amani na furaha na hatimaye kuwapo mafanikio katika kazi yake na taasisi kwa ujumla, ni lazima pia familia yake iwe na furaha.

Kama nilivyoeleza katika makala iliyopita, wafanyakazi wakiwa na matatizo ya kiuhusiano kazini na nyumbani, hali hii kwa sehemu kubwa huathiri kiwango cha furaha na utendaji wao wa kazi.

Kunapotokea matatizo ya ndoa na uhusiano kwa mfanyakazi, msongo wa mawazo ni lazima. Hii humwathiri mfanyakazi kisaikolojia, kiafya, kimwenendo na ufanisi katika utendaji wa kazi na hatimaye kusababisha hasara kwa taasisi.

Kwa mantiki hiyo, ifahamike kwamba ndoa au uhusiano huchangia kwa kiasi kikubwa matokeo ya utendaji kazi na ustawi wa taasisi. Kunapokuwa na matatizo katika ndoa au uhusiano, ni dhahiri ufanisi utakuwa mbovu. Pia kunapokuwa na furaha na amani katika ndoa au uhusiano, tija na ufanisi mahali pa kazi ni lazima vitapatikana.

Kutokana na ukweli huo, mfanyakazi anapokuwa na familia yenye furaha na amani, ni hakika mambo katika sehemu yake ya kazi yatakuwa mazuri. Kwa hiyo, ili mfanyakazi au mtumishi afanye kazi kwa ustadi na weledi, lazima apate muda wa kuwa karibu na familia.

Ndoa, kama tunavyoelewa, ni kiini cha familia, jamii na taifa. Hivyo, ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia, jamii na taifa imara. Ndoa imara huleta tija mahali pa kazi. Kazi na familia hutegemeana.

Hivyo, ili ndoa iwe na amani na furaha na pia kuwe na ufanisi kazini, ni lazima mtu atenge muda wa kazi na ule wa kuwa na familia. Kama nilivyodokeza katika makala iliyopita, kwani nguvu kubwa ikielekezwa katika kazi, kuna uwezekano mkubwa wa kusahau familia. Vivyo hivyo, nguvu kubwa ikielekezwa katika familia na kusahau majukumu ya kikazi, hili nalo ni tatizo.

Kutokana na hali hiyo, Ili kuwa na muda wa kazi kwa upande mmoja na familia upande mwingine, ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

Kwanza, kujali muda na kuacha kuishi kwa mazoea. Siku zote tatizo si muda, bali namna ya kutumia muda tuliopewa. Watu wengi wana tatizo la matumizi ya muda. Hakikisha muda wa kazi unautumia kwa kazi na siyo mambo mengine nje ya kazi. Zingatia muda wa kuingia na kutoka kazini.

Halikadhalika muda wa familia, utumike kwa ajili ya familia. Kwani lipo tatizo kwa baadhi ya wafanyakazi kutumia muda wa kazi kwa mambo mengine yasiyohusiana na kazi, hivyo, kujikuta muda ambao ungetumika kuwa na familia, unatumika kwa kazi za ofisini.

Pili, kujiwekea mipaka na vipaumbele. Si lazima kufanya mambo yote kwa siku moja, kwani hata kesho ipo pia. Jifunze kupangilia kazi zako kwa kuzingatia vipaumbele.

Tatu, kutunza nidhamu ya matumizi ya simu yako ya mkononi. Kuna baadhi ya watu ni watumwa wa simu zao za mkononi. Wakati wote wanashughulika na simu. Simu yako ya mkononi isiibe muda wa mwajiri wako au familia yako.

Ni muhimu kujua ni mahali gani na nyakati zipi za kutumia au kutokutumia simu yako. Pia jifunze au jenga mazoea ya kuitelekeza simu yako wakati mwingine ili usiharibu kazi na uhusiano wako na familia au mpenzi wako.

Nne, hakuna budi kujifunza kusema hapana. Usiwe mtumwa wa matukio au marafiki. Kila mahali unataka kwenda. Ukiambiwa twende huku au kule unakwenda. Hujui kukataa na huna vipaumbele. Kuna mambo ya kusema hapana.

Muda na familia yako niwa thamani sana. Pangilia muda wako kwani mumeo, mkeo, mtoto au watoto wako ni watu muhimu sana na wawe kipaumbele chako. Thamani yako kwao inategemea muda unaowekeza kwao.

Tano, tengeneza muda wa kuwa na familia. Muda usipotengenezwa hauwezi kuja. Dhamiria kutengeneza muda wa kuwa na familia. Tengeneza muda ili usiwe mgeni wa familia na nyumba yako kila siku. Kazi zisiwe kisingizio cha kudumu na kukosa muda na mwenzi wako au familia yako. Msingi wa familia ni pale wanandoa wanapopata muda wa pamoja.

Sita, nafasi zetu za kazi zibaki mahali pa kazi na si kwenda nazo mpaka nyumbani. Ukiwa nyumbani tambua kuwa wewe ni mke au mume wa mtu na baba au mama wa familia. Timiza wajibu wako wa nyumbani ili thamani ya uwapo wako iongezeke kwa mkeo au mumeo pamoja na watoto.

■ **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa na malezi. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz**

# MAISHA

DESEMBA 13, 2020

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 10

## Polisi pia hupenda watoto sikukuu



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Msimu wa Krismasi pendezesha nyumba kwa mapambo



## HARUSI

Ukurasa 12



## MATITI YA KUSIMAMA

# Mwonekano unaofurahisha wanawake

Ukurasa 14

# Polisi pia hupenda watoto sikukuu

**Na Moses Ismail**

WATAVAA nguo zao za sikukuu ambazo wanatamani sana kuringishia kwa wenzao, kabla ya hapo watakula chakula kizuri, watakunywa soda na juisi na hela za sikukuu pia watapewa.

Ndio, wanatarajia hivyo. Na kwa nini wasitarajie hivyo wakati wanajua wakati wa sikukuu kama ya kesho, Krismasi ni siku yao ya kula, kunywa, kuvaa nguo nzuri na kupewa hela za sikukuu?

Sio wao tu, hata wazazi wanatarajia watoto watafurahi hasa wakizingatia kuwa matayarisho yote ya sikukuu yamekamilika ikiwa pamoja na kuwanunulia nguo nzuri walizo chagua watoto wenyewe au walizo wachagulia.



Wazazi wanajua pia kuwa jioni lazima watoto watoke na kutembea sehemu mbalimbali kwa ajili ya kufurahia siku hiyo kubwa. Ni siku yao ya kutoka na kwenda 'kuinjoi' kwa uhuru mpaka.

Wapo watoto watakaotoka na wazazi wao na wapo pia watoto watakao 'ongozana' na 'wakubwa' zao kwenda kutembea sehemu tofauti kama 'bichi' kwa wale walioikaribu na bahari au kwenye maeneo yaliyotayarishwa sherehe za watoto.

Suala linabaki ni je, watoto hawa watarudi salama majumbani mwao baada ya 'kula sikukuu'?

Ndio, hilo ni suala la msingi ambalo kila mzazi anapaswa kujiuliza kwa kuzingatia kuwa uzoefu unaonyesha kuwa mbali ya sikukuu kuwa ni siku ya furaha kwa watoto, lakini mara kadhaa hutokea matukio mabaya ya kusikitisha.

Yapo matukio ya mabaya yanayokumbukwa kutokana kujirudia kila sikukuu kubwa kama ya watoto kuzama na kufa maji, kugongwa na magari, kupotea na hata kufa kwenye kumbi za muziki uliotayarishwa ka ajili ya watoto.

Matukio ya aina hiyo hayafurahishi hata kidogo na yanaleta huzuni kwa jamii nzima na kuwachia wazazi wa watoto wanaopatwa na mikasa hiyo majonzi yanayojirudia kila ijapo sikukuu iliowaondolea mtoto au watoto wao.

Kwa kutambua hayo na kutaka kudhibiti yasijirudie, serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikitahadharisha umma kuwa makini na nyendo za watoto hasa waendao maeneo ya ufukweni na kwenye nyumba za starehe.

Tahadhari inayotolewa na polisi kila mkoa, kutegemea na mazingira ya maeneo ya watoto 'kula sikukuu', si ya kuchukulia kiwepesi, hutolewa kwa kurudiarudia kwa kuzingati uhalisi wa matukio mabaya nyakati za sikukuu.

Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kwa mzazi kuwasisitizia 'watoto wakubwa' kuwa waangalifu na makini kwa wadogo zao wakati wa matembezi na pia kuwasisitizia pia wasijaribu kuogelea baharini hata kama wanajua kuogelea.

Polisi huwapenda zaidi watoto wakati wa sikukuu na maagizo yao yakifuatwa inatawezekana kwa asilimia nyingi tu wazazi kuwaona watoto wao wakirudi salama majumbani baada ya sikukuu, na yakipuuzwa huenda ikawa kinyume.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Weka vivumishi vifuatavyo, vya lugha ya kifaransa, katika umoja.**

• Des affaires régionales.
**Une affaire régionale**

• Des organismes nationaux.
**Un organisme national.**

• Des problèmes culturels.
**Un problème culturel.**

• Des histoires exceptionnelles.
**Une histoire exceptionnelle.**

• Des sites merveilleux.
**Un site merveilleux**

• Des propositions sérieuses.
**Une proposition sérieuse**

• Des journaux français.
**Un journal français.**

• Des journalistes françaises.
**Une journaliste française.** Pia, unaweza kusema **Un journaliste français.**


Weka kivumishi kionyeshi katika maneno yafuatayo kwa kuondoa "article". Katika kufanya hivyo, zingatia jinsia ya kila neno.

Kwa mfano: **La fille - cette fille**

- Le métro – ce métro
- La voiture – cette voiture
- La moto – cette moto
- Le train – ce train
- L'avion – cet avion
- Le compartiment – ce compartiment
- Le taxi – ce taxi
- Le wagon – ce wagon
- L'autobus – cet autobus
- La mobylette – cette mobylette

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

Kijana mmoja alikwenda sokoni kununua nyanya, hali ilikuwa hivi!

Kijana: Nyanya zinauzwa kiasi gani?

**Muuzaji:** Kilo shilingi 1500

**Kijana:** Lakini nataka unisagie. nataka kwenda kula na chipsi nyumbani

**Muuzaji:** Kijana usitanie kazi za watu, kwenda hukoo

Swali
Mnyama Nyumbu anapatikana wapi kwa wingi?

# MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



## Chanzo cha matatizo ya ndoa ni sisi wenyewe na vizazi vyetu

MSOMAJI wangu, bado naendelea kuchambua chanzo cha matatizo mengi katika familia zetu. Wiki iliyopita nilielezea vyanzo viwili ambavyo ni nguvu ya giza na dhambi.

Nikasema matatizo mengi yanayotikisa maisha yetu yanasababishwa na roho asi zilizoachiliwa kwenye ulimwengu wa giza. Pia nikataja dhambi kuwa chanzo kingine ambacho ama imefanywa na sisi wenyewe au wazazi/babu/bibi zetu na sasa adhabu zinatupata.

Katika maandiko matakatifu, kuna maneno yanasema: "Baba zetu walitenda dhambi, hata hawapo, na sisi tumeyachukua maovu yao". Hebu sikia yanayotokea yakisababishwa na mababu au mabibi zetu.

Nilisema wiki iliyopita kwamba maovu ni matunda ya mti dhambi. Kile unachokitenda leo, kinaweza kugharibu kizazi chako chote. Leo hii unateseka ni kwa sababu ya yale yaliyofanywa na wazazi wetu.

Yupo dada mmoja rafiki yangu nikamuuliza kwanini yupo katika hali ile niliyomuona na umri wake na umri wake ni mkubwa. Akaanza kunisimulia akasema kwao wamezaliwa sita.

Akasema bibi yao kizaa mama yao aliolewa, akaachika. Akaolewa ndoa ya pili akaachika, akaolewa ndoa ya tatu napo akaachika. Akaenda akaolewa ndoa ya nne. Watoto alikuwa nao wa kuwazaa 11.

Katika watoto hao 11, watatu ni wa kiume. Akasema hao wajomba zake, yule wa kwanza alifunga ndoa lakini ana watoto sita nje ya ndoa. Kila mtoto na mama yake.

Akasema mjomba wake mwingine alikuwa akioa na kuacha mwisho akaoa mwanamke mwisho akafa. Mjomba mwingine kadhalika alioa lakini akaacha.

Mama zake wakubwa na wale wadogo wote wanane hakuna aliyeolewa kwa ndoa. Wote walikuwa wakiolewa mke wa pili, mke wa tatu au anaishia kuzaa tu hapo nyumbani kwao.

Akasema, kwa mama yao walizaliwa sita lakini kila mtoto na baba yake. Na kwamba ukichukua watoto wote wa mama mkubwa na wa mama mdogo, wale wa mjomba, endapo itatokea ameolewa, kufunga ndoa, miaka mitano ni mingi ndoa inavunjika.

Au kama ni mwanamume, atafiwa mke na kama ni mke atafiwa na mume. Au ataachika kwa sababu ya uzazi umegoma au watazalia tu nyumbani. Na hapo chanzo ch tatizo ni yule bibi aliyeolewa mara nne.

Unaweza kuwa unapigana kuangalia imekuwa hivi, mbona mambo hayaendi. Rudi nyuma kwenye chanzo. Mashangazi zako, wajomba, mama zako, je, walidumu kwenye ndoa? Bibi alidumu kwenye ndoa? Ni kweli babu alikuwa na mke mmoja, lakini yawezekana alikuwa na watoto wengi pembezoni.

Hapo tayari unaingia kwenye mnyororo wa ndoa za mitala(wake wengi). Utang'ang'ana kuvumilia lakini utaishi kwa mateso. Lengo la hizi roho ni kwamba utoke ili uende kwingine. Au ukijilazimisha sana unaishia kufiwa.

Yupo mtu mmoja aliletwa kanisani nikaambiwa niongee naye. Wakati tunaongea akasema", nilikuwa hivi kwa sababu mume wangu alikuwa na upungufu kadhaa. Kila mfanyakazi anayekuja pale nyumbani, basi yule ni halali yake".

Mpaka sasa mama huyu amechoka na ndoa iliyomsababisha apate vidonda vya tumbo, presha ya macho hadi kufikia lensi ya mwisho.

Lakini nikamwambia anipe historia ya mama yake na ukoo wake. Pia historia ya baba. Ilikuwa ni kituko.Mpaka kufikia kile kizazi cha mume wake, kuna vizazi kama sita vilivyopita. Vyote vimevuruga katika mtindo huo.

Mpaka kufikia mume wake anasema kwamba mama mkwe wake mumewe alikuwa akiishi kwa dadayake. Yule shemeji mtu akamkamata kwa nguvu ikapatikana mimba ya mume wake.

Nikamwambia dada hata leo ikitokea umekufa, kizazi chako kipo kwenye mnyororo huo, huwezi kukwepa. Na kama huhutashughulika na chanzo cha tatizo, unaweza ukafa leo lakini kizazi chako ambacho kipo kwenye huo mnyororo itakuwaje?

Ni heri wewe uliyeijua neema ukaanza kushughulika kukomboa uzao wako. Unachofanya leo chaweza kuwa faida au hasara kizazi chako chote.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kuhusu chanzo cha matatizo ya wengi wetu. Inawezakana kabisa mifano hiyo niliyozungumzia hapo, hata wewe yapo matukio yanayofanana na hayo. Chimbua chanzo kisha chukua hatua mapema kuokoa warithi wako.

Kwa leo naishia hapa. Naamini umejifunzo kitu hapo. Ukiwa na maoni, ushauri au kisa usisite kunitumia ujumbe kupitia 0715268581. Hadi wiki ijayo.

# NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



## Ushirikiano taasisi za uhifadhi suluhisho ujangili mpya wa tembo

HIVI karibuni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), lilieleza kuwapo kwa aina mpya ya ujangili kwa kisingizio cha maini na mafuta ya tembo hutibu saratani na vidonda vya tumbo.

Imani hiyo imepandikizwa kwa wananchi na watu wasio na nia njema kwa rasilimali wanyama, kwa kuwa wananchi kwa njia mbalimbali wanaua wanyama hao na majangili wanachukua meno ya tembo.

Wananchi wameaminishwa kuwa maini ya tembo hutibu saratani ya ini na kizazi kwa wanawake, lakini pia vidonda vya tumbo na wengi wamejikuta wakiingia katika kuteketeza rasilimali za nchi kwa manufaa ya wanaochukua pembe.

Hali hiyo inatokana na tembo kutoka maeneo yaliyohifadhiwa kwa sababu mbalimbali kama kutafuata maji hasa wakati wa ukame au kusafiri kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kupitia kwenye mapito yao ambayo hujulikana kama shoroba.

Kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu, shoroba nyingi zimefungwa kwa kuwa wananchi wamfungua mashamba, wamejenga makazi na shughuli zingine kiasi cha tembo wanapopita kwenye njia yao ya asili wanaishia kwenye migogoro na binadamu.

Utafiti unaeleza kuwa tembo ni mmnyama mwenye kumbukumbu kubwa kwa kuwa huweza kukumbuka na kupita njia aliyopita za wazazi wake miaka 100 iliyopita.

Wakati wanapita katika njia hiyo, wamejikuta katika migogoro kwa kuwa binadamu hutegesha misumari na kuweka sumu kwenye maboga yanayoliwa na tembo ambao hufa na wananchi hushambulia mzoga kwa lengo la kupata maini na mafuta ya tembo.

TANAPA haijatoa takwimu za tembo waliouawa pamoja na maeneo ambako matukio hayo yametokea lakini inaeleza kuwa ni mengi ambayo yanatishia uwapo wa rasilimali hiyo.

Kwa takribani miaka miwili, hakuna ujangili wa tembo kwa lengo la kupata kinachodaiwa ni dawa. Pia tangu TANAPA iwe na jeshi la uhifadhi au jeshi usu imesaidia mabadiliko ya mapambano dhidi ya ujangili kwa kuwa sasa zinatumika silaha za kivita na teknolojia kama ambavyo majambazi wanafanya.

TANAPA ni ya taasisi nyingi zinazohusika na uhifadhi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ambazo zina wajibu wa kulinda rasilimali wanyama na misitu.

> **TANAPA haijatoa takwimu za tembo waliouawa pamoja na maeneo ambako matukio hayo yametokea lakini inaeleza kuwa ni mengi ambayo yanatishia uwapo wa rasilimali hiyo.**

Nawaza kuwa bila ushirikiano wa dhati na pamoja kwa taasisi hizo TANAPA haitaweza kupambana katika vita hii mpya, kwa kuwa yenyewe inahusika na usimamizi wa hifadhi za taifa 22, lakini wanyama wanapotoka nje ya hifadhi wanakuwa chini ya uangalizi wa taasisi nyingine.

Mathalani, TANAPA inasema eneo la ikolojia ya Selous ambako kuna Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, ujangili wa tembo ni mkubwa. Wanyama wanapotoka hifadhini kwenda kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na jamii (WMA) wanakutana na vikwazo kwa kuwa maeneo hayo yapo kisheria lakini hakuna utunzaji.

Ni lazima wanyama hao kutoka hifadhini humo kwenda Pori la Akiba Selous na baadaye Msumbiji ambako kote bado hakuna udhibiti wa kuwezesha usalama wao.

Inaelezwa kwa sasa kuna shughuli za kijamii zinaendelea katika ikolojia ya Nyasa Selous yenye ukubwa wa kilomita za mraba 160, kwa makundi makubwa ya wafugaji kuweka makazi huku wakivuna miti kwa kasi, pamoja na wakimbizi wa Msumbiji.

Bila ushiriki wa taasisi hizo tembo hawatabaki salama kwa kuwa sasa nguvu ya wananchi walioaminishwa kuwa watapano maradhi hayo ni kubwa na wanatumia mbinu nyingi za asili kuwapata wanyama hao.

Ni muhimu taasisi hizi zikashirikiana vyema kutoa elimu kwa umma na kutoa ushahidi wa kisayansi kuwa hawawezi kupona maradhi hayo kwa kutumia maini au mafuta ya tembo. Hakuna ubishi kuwa meno ya tembo soko lake kubwa ni nchi za Asia yaani Thailand, China na Vietnam ambazo bado hazijaonyesha utayari wa kuwa na sheria kali dhidi ya biashara hiyo.

Kichocheo kikubwa cha biashara hiyo ni imani na utamaduni kuwa viungo vya wanyama hao hutibu magonjwa mbalimbali kama homa, kupooza, huku wengine wakitaka kuwa na bidhaa zilizotengenezwa kutokana na pembe ya faru au meno ya tembo kama ufahari na heshima katika jamii, na wengi hutumia fedha nyingi ili kupata viungo hivyo.

Ushirikiano wa dhati chini ya utayari wa kisiasa uliopo nchini kwa sasa ndiyo msaada mkubwa katika kulinda rasilimali hii muhimu inayoliingizia taifa fedha za kigeni.

***Tutafakari!***

***Mungu ibariki Tanzania.***

# HARUSI









Ilikuwa shangwe na vigeregere katika sherehe ya kumuaga binti yao kipenzi, Augusta Njoji, iliyofanyika jijini Dodoma, mwishoni mwa wiki. Augusta ni mfanyakazi wa kampuni ya The Guardian Ltd.



# MITINDO







UNENE SI TATIZO

## Ukijikubali kimavazi, utapendeza

KUNA tatizo la wanawake wenye maumbo makubwa kujiona wao kama viumbe wasio na bahati ya kupata mavazi yanayowang'arisha, kama walivyo kwa wenye maumbo ya kawaida.

Wengi huona ni vigumu kupata nguo ambazo hata wao watajisikia wamependeza.

Hali hiyo, husababisha kuwa na hofu, msongo wa mawazo na kutojiamini, hata kama wamevaa nguo zilizowatoa vyema.

**NAMNA YA KUFANYA**

Unatakiwa kuukubali mwili wako, sema kwa sauti ukiwa peke yako " huu ni mwili wangu,unaonifanya nionekane mtu hapa duniani, unene sio kilema, nashukuru Mungu kwa kuniumba hivi."

Rudia maneno haya kila wakati pale wanapojihisi kutojikubali.

**UNAPENDEZA UKIVAA**

Siri moja ambayo watu wa aina zote wanayo katika kuvaa ni kuvaa nguo zinazokutosha vizuri na unazojisikia huru.

Usinunue nguo za kukubana sana au isiyokutosha kabisa ili mwili wako uonekane vizuri.

Pia usivae nguo pana kuliko unene wako, eti kwamba imani kwamba nguo pana zote zinakuhusu. Nunua ukubwa unaokutosha vizuri na ikiwezekana inayokwenda na wakati.

Kumbuka kwamba namna unavyojipenda na kupangilia mavazi yako yatakusaidia uonekane mpya, usiyezeeka na mrembo kila siku.

Si lazima uwe na pesa nyingi kwa ajili ya kupendeza, lakini kikubwa zaidi kitakachokusaidia ni kutambua mwili wako vizuri na ubunifu katika kutafuta nguo zinazoendana na wewe.

## UREMBO







MATITI YA KUSIMAMA

# Mwonekano unaofurahisha wanawake

IDADI kubwa ya wanawake wanakosa furaha pale wanapoona kiungo muhimu kama matiti yanapoteza muonekano wa kupendeza baada ya kukosa nguvu na kuanguka.

Kiungo hiki ni muhimu katika urembo wa mwanamke mara nyingi yanapokuwa katika hali ya kusimama, utafsiriwa ni alama ya mvuto na urembo kwa mtu huiska.

Bahati mbaya, matiti yanapofikia muda fulani huanguka kutoka hali yake ya awali ya kusimama, hivyo huwapatia changamoto baadhi wa wanawake wanaopenda kuonekana kijana kila wakati.

Hata hivyo, inakuwa vigumu kurudisha katika hali hiyo, kwani muda wake ukifika wa kuwa hivyo, basi inambidi mtu kukubali matokeo.

Kuanguka kwa matiti inatokana na sababu kuu mbili, kwanza pale yanaponyonywa na watoto, na pili umri unapozidi.

Kutokana na sababu hizo, baadhi ya wanawake wanakataa kuzaa mapema na wengine kushindwa kunyonyesha watoto wao wakihofika kuathiri matiti yao.

Kupitia safu hii utapata mbinu rahisi ya kurejesha furaha yako kwa kuyafanya matiti yasimame tena.

**FANYA MAZOEZI**

Kama matiti yako yamelala, unaweza kuchukua mazoezi maalumu ya kusisimua misuli, mtafute mtaalamu wa mazoezi ambaye atakupa mazoezi ya kuimarisha misuli ili matiti kuwa na nguvu kama zamani.

**MASAJI YA BARAFU**

Chukua kipande cha barafu na kisha jichue taratibu kuzunguka matiti yote.

Aina hii ya uchuaji ukifanya kila mara, inasaidia kuimarisha misuli na kuwezesha kurudi kama ilivyokuwa awali.

**MAYAI**

Mchanganyiko wa mayai, vitamini E na maziwa ya mtindi unasaidia kukurudishia matiti ya ujana.

Unatakiwa kupaka mchanganyiko wako kwenye matiti na kisha jichue kila siku wakati wa kulala.

## MAPISHI

### Na Mary Geofrey

# Juisi ya Malimao





KINYWAJI hiki ni rahisi kuandaa na ni kizuri kwa afya zetu.

Limao na tangawizi husaidia mwili kupata virutubisho na vitamini mbalimbali mwilini.

Epuka kutumia sukari nyingi maana si nzuri kwa afya, ukiweza tumia asali kiasi.

**MAHITAJI**

Malimao fresh sita, asali kikombe 1, tangawizi iliyokwanguliwa nusu kikombe, maji vikombe 2 maji ya baridi vikombe 14

**NAMNA YA KUANDAA**

Chukua bakuli safi, kwenye bakuli kamua malimao kisha toa mbegu zote, yabaki maji ya limao.

Washa jiko, bandika sufuria weka vikombe 2 vya maji, asali na tangawizi.

Acha mchanganyiko uchemke kwa moto mdogo kwa muda wa dakika 10, mpaka asali iyeyuke na harufu nzuri ya tangawizi isikike.

Epua, acha ipoe, chukua jagi safi, kwenye jagi, weka maji ya limao, maji ya baridi vikombe 14 kisha weka mchanganyiko ulioutoa jikoni.

Changanyanya vizuri kisha weka kwenye jokofu kwa muda wa saa moja.

Kama utapenda weka majani ya mnanaa na giligilani ili kupata harufu nzuri.

Juisi yake itakuwa tayari kunywa baada ya kupata mlo wako safi au wakati umepumzika na familia.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Msimu wa Krismasi pendezesha nyumba kwa mapambo

MSIMU wa sikukuu umewadia, huku kukiwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba, kukiwa kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Katika ofisi na sehemu mbalimbali ukipita au kuingia unakutana na mapambo ya sikukuu ikiwamo mti wa Krismasi.

Leo tunakupa dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitasaidia kuifanya sikukuu yako kuwa nzuri, ukaifurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba katika kipindi hiki familia nyingi huwa zinaungana pamoja katika mapumziko ya mwisho wa mwaka, kwa hiyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa ni cha furaha zaidi kwa mapambo tofauti ya sikukuu ndani ya nyumba.

Pia, yapo mapambo mengine tofauti hilo, kama hutoweza kupata mti, unaweza pia kutafuta aina nyingine ya mapambo ambayo huenda yasikugharimu kabisa au ukayapata kwa gharama kidogo.

Lengo ni kuhakikisha nyumba yako inachangamka na kuipa raha familia ambayo imekusanyika nyumbani kwa ajili ya mapumziko.

Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wall papers' na mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na sikukuu pamoja na maua.

Mapambo mengine ambayo yanaweza kutumika Krismasi ni pamoja na karatasi za rangi, taa za kung'aa, mapambo ya karatasi yanayotengenezwa kwa mtindo wa nyota.

Mengine ni kengele za Krismasi, picha za kondoo, farasi, mipira ya kung`aa, wanyama wadogo wa kutengenezwa kama kondoo.

Pia, unaweza kutengeneza maua ya asili kwa kuyaweka katika chombo au chupa maalum ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.

Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.

Unaweza kupamba pia maneno yenye ujumbe maalum unayoweza kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalum yanapopatikana.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Nyumba katika musimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa msimu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya muonekano wa nyumba yako.

## MPANGILIO

### Dondoo jinsi ya kupamba kabati la vyombo msimu wa sikukuu

**1:** Tandika kitambaa cha mapambo juu ya kabati. Unaweza kuwa na kitambaa cha rangi au michoro unayoipenda na ukakitandika juu ya kabati la vyombo.


**2:** Weka vishikio vya mishumaa, kadi na vitu vya msimu wa sikukuu.

**3:** Weka vitu kama magamba ya samaki au vitu kale juu ya kabati.

**4:** Weka stika yenye michoro ya matunda au rangi za kupendeza katikati ya vioo au pembeni ya milango.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
NINAWASALIMU SINA KINYONGO NAJUA MLIKOSEA KUTONIPIGIA AU SIOOOOO?
SIO HIYO KWIOOOO..
JUKWAANI
HIVI KIINUA MGONGO KINA UDUGU GANI NA 'STROKU?'...MAANA KIKIONDOKA INAKUJA STROKU!
NIMEGOMBEA UPANDE HUU NIKAKOSA,...ETI NIPEWE KITI IKULU NINGEWAKATALIA 'KATA KATA!' LABDA WAIF' ANGENAMBIA NENDA.
WEEEEE! KISEBUSEBU
UNATATUA MIGOGORO YA NDOA LAKINI JE, WEWE NDOA YAKO IMETULIA?
AH! WAPI... INAYUMBA KAMA DISHI BOVU!
ULAJI UMEOTA MBAWA ULEEEEEEE...SIJUI NANI ALILISHIKILIA BANDO LANGU LA SAUTI MPAKA NIKAPATA KIGUGUMI...
ULIPOKWENDA HUKO ULIAMKA HAPA KWANGU AU SHOBO?
YALIYOPITA SI NDWELE TULIDHANI HAITATOKEA SIKU TUKAWA URAIANI... TUPANGE TUNAISHIJE?
UNAJUA TUSIPOKUWA MAKINI TUTAGOMBANIA RIMOTI NA WATOTO?
WEWE ULIKUWA MTU MKUBWA MBONA SASA UNAFANYA MAMBO YA KITOTO?
UNASHANGAA NINI WAKATI UKIWA MKUBWA LAZIMA URUDI UTOTONI!
WAHENGA WAKULU NA WAKULUNGWA KIJANA WENU KAJA NAMBIENI SHIDA YAKE....?
MNASEMA ALIKUWA ANAWATIMULIA VUMBI HATA NYIE WAKULUNGWA HAKUWATHAMINI.... AJIANDAE KUWA FUNDI VIATU....
"NANI KASEMA???
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...YUMBA KIMAISHA UWAONE WABAYA WAKO...

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za kazi ya ualimu Diploma**
**- Kiswahili**
**-Science SST**
**- Kiingereza**
**Mawasiliano:**
**0783 334653**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA.11/2020**

**ANDHER..........BALJIT SINGH..........**
**MAREHEMU**
**NA**
**PANDHER..........RAJBIR BALJIT..........**
**MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75 na 76)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya Usimamizi wa Mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **tarehe 14** Mwezi Desemba Mwaka wa **2020**. Imewasilishwa leo **tarehe 27 Mwezi Desemba** Mwaka wa **2020.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGITRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**MISC. LAND APPLICATION NO.58 OF 2020**

(C/f The High Court of Tanzania at Arusha Land Appeal No 20 of 2017 and Original Karatu District land and Housing Tribunal application No 22 of 2008)

**..........JOSEPH LOHAY AKUNAAY..........**
**APPELLANT**
**VERSUS**
**MAGHWAY..........PASKALI CLET..........**
**RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**
**TO: PASKALI CLETI MAGHWAY.**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention in the HIGH COURT at Arusha on **24th** day of February, **2021** at 09:00am in the forenoon.

**YOU** may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention, the court may proceed in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of the **COURT** this **16th** day of November,**2020**

**R.B.MASSAM**
**DEPUTY REGISTRAR**
**ARUSHA.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**

**MJINI-MOROGORO**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NO;369/2020**

OMBI LA **MOHAMED HAMISI MWAMPEPO**,KUTEULIWA MSIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU **RAMADHANI SELEMANI MTALISUSU**. WATU WOTE WANAODAI KUWA NA UHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU KUWA WANAARIKWA KUJA NA KUUDHURIA SHAURINI MNAMO TAREHE **22/12/2020** KABLA YA MUOMBAJI HAJATEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.WOSIA YA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA TAREHE **04/12/2020.**

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

NINAUTANGAZIA UMMA KUWA, KWA AMRI YA MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI, WILAYA YA DODOMA NITAUZA KWA MNADA KIWANJA KILICHOPO MKONZE MALI YA PASCHAL MWANDU KIDALABYA ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA KAMO MICROFINANCE LIMITED. MNADA UTAFANYIKIA KIWANJA KILIPO NA KITAUZWA KAMA KILIVYO SIKU YA TAREHE 24/12/2020 SAA NNE 4:00 ASUBUHI.

- WATEJA WATASHINDANA HADHARANI, MWENYE BEI YA JUU ATATANGAZWA MSHINDI.
- MTEJA AKISHANUNUA, GHARAMA ZA KUBADILI UMILIKI NI JUU YA MTEJA.

**KARIBUNI NYOTE, USISITE KUWASILIANA NASI KWA MAELEKEZO ZAIDI KUPITIA SIMU NAMBA 0735 170 553 (DALALI WA MAHAKAMA)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:303..2020**

**Mdai: RAPHAEL PASCAL SIMBA**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: SAIDI HAMADI**
**Kwa: SAIDI HAMADIWA MODECO-MOROGORO**

**Ombi la Mdai: RAPHAEL PASCAL SIMBA**
**Madai ya: PIKIPIKI MOJA AINA YA HAOJUE MC 417CPZ**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **tarehe 14 mwezi 12 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi**.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa / mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo **tarehe 08 mwezi 12 mwaka 2020.**





**UZA,**
**CHENYE THAMANI KUBWA KWA KUTANGAZA NASI KWA BEI POA**
**TUPIGIE 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA

# Barua ya wazi kwa Waziri wa Elimu



Na Magabilo Masambu

**Mpaka leo sijaelewa kwanini masomo yalichanganywa, kwa maana ya kuwa na somo la maarifa ya jamii! Zamani tulisoma kila somo kivyake Jiografia, Historia, Sayansi kilimo, sayansi kimu, nakadhalika. Utaratibu huu ulimfanya mwanafunzi asome somo kwa undani zaidi na kumwezesha kuwa na fikra pana na uelewa mkubwa.**

**Salaam ndugu Waziri!**

KWANZA nikupongeze kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena, kama Waziri wa Elimu, hongera sana mama. Si jambo jepesi sina mashaka na uzoefu wako.

Nitumie ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa maoni yangu juu ya mfumo wa elimu yetu, ili ikikupendeza uweze kuchukua hatua. Tusiendelee kukosea kama navyoamini sasa, kwamba kuna jambo halijakaa sawasawa.

Kumekuwapo na maoni tofauti juu ya wahitimu wa kada mbalimbali za elimu juu ya fikra zao. Walio wengi wanalaumiwa kuwa uwezo wao wa kufikiri na kupambanua mambo ni mdogo kuliko ufaulu wao katika vyeti.

Lazima nikiri kwamba sjawahi kufanya utafiti kuhakikisha hilo. Lakini waswahili wanasema lisemwalo lipo, kama halipo laja! Inawezekana ni kweli na kama ni kweli, lazima itafutwe dawa, ili tuwe na wasomi ambao matokeo yao ya mitihani yanafanana na waliyonayo vichwani si wote ila inaonekana ni asilimia kubwa wako hivyo.

Ni ukweli uliowazi kwamba, leo hii ukimchukua mwanafunzi aliyemaliza darasa la nne la mkoloni na mwanafunzi wa leo wa chuo kikuu, ukawaweka mahali bila kufahamu viwango vyao vya elimu, ukawaambia wajieleze pengine huyu wa darasa la mkoloni ataonekana ndiye aliemaliza chuo kikuu kunashida!

Elimu yetu imepitia katika mabadiliko mengi na kila waziri anapoingia anaona ili aonekane amefanya kitu ni kuweka mabadiliko hata kama yatakuwa na athari, kwake yeye ni mabadiliko na kwamba kapiga kazi.

Elimu yetu hasa ya msingi imekuwa kama sahani ya chakula katika sherehe! Sahani ambayo unawekewa mchanganyiko wa vyakula unakuta pilau, wali mweupe, ngogwe, bamia, ndizi za kukaanga, viazi. Vyote huwekwa kidogo kidogo ndivyo elimu yetu ya msingi ilivyo.

Mpaka leo sijaelewa kwanini masomo yalichanganywa, kwa maana ya kuwa na somo la maarifa ya jamii! Zamani tulisoma kila somo kivyake Jiografia,

kimu, nakadhalika. Utaratibu huu ulimfanya mwanafunzi asome somo kwa undani zaidi na kumwezesha kuwa na fikra pana na uelewa mkubwa. Hapa ndipo tatizo lilipoanzia turudi tulikotoka.

Kitu cha ajabu ni kwamba wanapofika shule za sekondari wanakwenda kusoma somo moja moja, yaani sasa msingi umeshakuwa mbovu unapauwa kwa kutumia mawe. Kwahiyo unakuta wanasoma kwa kukariri ili wafaulu mitihani.

Jambo baya zaidi ni juu ya somo la kilimo. Asilimia kubwa kama si zote wananchi wa Tanzania ni wakulima na kilimo ndiyo sekta iliyobeba watu wengi zaidi hasa wananchi wa kawaida, lakini sina hakika kama somo la kilimo lipo shule za msingi kama ilivyokuwa zamani sayansi kilimo.

Uholanzi ni nchi iliyojengwa chini ya usawa wa bahari na karibu nchi mzima imezungukwa na maji, kwa kulijua hilo wakaamua kuingiza kwenye mtaala kwamba kila taasisi ya elimu lazima kuwapo mabwawa, wanafunzi wafundishwe kuogelea, ili siku ikitokea nchi imezama kila mmoja aweze kujiokoa.

Somo la kilimo limebaki kama somo la hiari katika nchi ambayo uchumi wake unategemea kilimo tutafika kweli? Tunatangaza serikali ya viwanda itawezekana bila malighafi? Au tunazungumzia viwanda vya chuma tu? Maana kama tunataka viwanda vitakavyowasaidia wananchi wa kawaida lazima wananchi wafahamu namna nzuri ya kuzalisha malighafi bora.

Kwa msingi huu somo la kilimo linatakiwa kuwa la lazima kutoka shule za msingi mpaka kidato cha nne. Imewezekanaje somo la historia linakuwa la lazima tena siyo historia ya Tanzania basi ni historia ya kikoloni halafu elimu ya kilimo ambayo ilitakiwa kila mtu aipate inakuwa ya kuchagua?

Wasiwasi wangu ni juu ya walimu wa kilimo, kadri siku zinavyokwenda hawatakuwepo tena, maana wanafunzi wanaosoma kilimo ni wachache sana na shule ni za kuhesabu.

Mwisho elimu ndiyo sekta mama, sekta nyingine zote hazipo kama hakuna elimu bora. Hatua za makusudi zisipochukuliwa kuna siku tutapata wasomi wa chuo kikuu wasiojua kusoma na kuandika.

Ni muhimu matokeo ya ufaulu kwenye vyeti yaakisi akili za wahitimu. Hili litawezekana kwa kurudisha mfumo wa zamani katika shule za msingi. Ninayo mengi nikipata nauli nitakuja tutete! Nakutakia kazi njema.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kwaheri Nzayadio, ahsante kwa kutuchezesha Cavasha



Na Adam Fungamwango

**"Oo tango mosusu ndoki yeye, ooo tangu masusu ndoki Maluku, tango mosusu soki Nzaya, ndoki Nzaya, tango mosusu ndoki tonelo, ndoki Tonelo, ndoki Tonelo, tango mosusu ndoki bino, ndoki bino."**

BURUDANI iliyotikisa leo inamwangazia mwanamuziki nyota kabisa wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kuanzia miaka ya 1970 hadi mwishoni mwaka miaka ya 1980, Nzaya Nzayadio.

Mwanamuziki huyo alifariki dunia Hull City, Uingereza Desemba 7, mwaka huu, kwa ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona, akiwa na miaka 65.

Vijana wa sasa wanaweza kushangaa na kuanza kujiuliza mara mbili mbili ni nani, lakini wale waliokuwa vijana au watoto miaka hiyo, sijui kama hawazifahamu nyimbo zilizokuwa zikitamba wakati huo zikiimbwa kwenye baa, magari, hoteli na hata vituo vya usafiri kama 'Kendeke Malembe eee eee na Lavi Malembe, Ngai Mama Nakoloba.'

Hayo ni baadhi ya maneno ambayo yamo kwenye wimbo wa 'Kendeke Melembe'. Ni moja ya kazi nzuri za mwanamuziki huyo.

Wale watoto wa Dar es Salaam miaka hiyo au waliowahi kuishi wakati huo ambao kwa sasa ni watu wazima na wametapakaa nchini hata nje ya nchi watakumbuka kulikuwa na gari moja linafanana na Hiace hivi, lilikuwa likizunguka jiji zima likiuza 'Ice Cream' aina ya koni na hata zile za kwenye vikopo vidogo vya pastiki, nyimbo za Cavasha ambazo nyingi zilikuwa ni za Les Kamale, Orchestra Kiam na Orchestra Lipua Lipua zilikuwa zikitawala kwenye gari hilo.

Watoto wakisikia nyimbo hizo tu, basi wanaanza kuomba pesa kwa wazazi wao au kulia, ili wanunuliwe koni.

Sauti ya Nzaya Nzayadio ndiyo ilikuwa ikisikika zaidi kwenye nyimbo nyingi, akiwa na Orchestra Lipua Lipua.

Ni mwanamuziki raia wa Congo aliyezaliwa mwaka 1955, lakini mashabiki wa muziki wa Tanzania wa wakati huo hasa wa Cavasha walimtambua kutokana na nyimbo zao nyingi kutamba nchini hata kwenye harusi, kumaliza shule, sikuukuu mbalimbali na hafla za chama na kiserikali.

"Oo tango mosusu ndoki yeye, ooo tangu masusu ndoki Maluku, tango mosusu soki Nzaya, ndoki Nzaya, tango mosusu ndoki tonelo, ndoki Tonelo, ndoki Tonelo, tango mosusu ndoki bino, ndoki bino."

Ni baadhi ya maneno maarufu sana kwa Wabongo kwenye wimbo wa 'Ndukidi' ambao Wabongo nao walikuwa wakiweka maneno yao ya kiswahili wanayojua wenyewe, ili mradi tu na wao wafurahi.

Hiyo ilikuwa sauti nzito ya Nzaya Nzayadio ambaye alikuwa akiitikiwa na mwimbaji mwenye sauti ya kwanza kali, Kilola Tokodiangani ambaye yeye bado yupo hai.

Lakini pia wabongo wanamkumbuka kwa wimbo wa 'Sekizengi' ambao unapoanza tu, anaanza kwa kusema 'Nzaya Nzayadio na Sekizengi'. Pia mwanamuziki huyo akiwa na bendi ya Lipua Lipua, ametunga au kuimba nyimbo nyingi akizotunga mwenzake zilizolipatia umaarufu sana kundi hilo na kuwa tishio.

Mbali na Kilola Tokodiangani, lakini pia alishirikiana na wanamuziki kama Lusuama Aspro na Mongoley Santana kwenye gitaa la solo na mchawi wa gitaa la rhythm na mtunzi wa nyimbo nyingi maarufu za bendi hiyo, Vata Mombasa 'Jujuman', Maluku na wengineo.

Nyimbo zingine zilizotamba sana akiziimba marehemu kwa umahiri mkubwa ni 'Mfueni', 'Matoba', 'Mbondo', 'Naleli Libala', 'Lemba Lemba',' Temperature, 'Nouvelle Generation' na zingine nyingi.

Mwanamuziki huyo, kabla ya kufariki dunia, alilazwa kwa wiki mbili kwenye Hospitali ya Hull Royal Infirmary, Hull City, akiugua ugonjwa huo ambao mpaka sasa bado ni janga la dunia.

Ana historia kubwa kwenye ulimwengu wa muziki, lakini umaarufu wake ulianza mwaka 1973 alipojiunga na Orchestra Lipua Lipua kwenda kuziba pengo la sauti nzito ya Pepe Kalle aliyekuwa amejiengua na kwenda kuunda bendi yake ya Empire Bakuba, akiwa na Papy Tex na Dilu Dilumona.

Pia Nyboma mwenye sauti ya kwanza aliondoka na kuchukuliwa Kilola Tokodiangani kuziba pengo pia na kuanza kuuwasha moto.

Ni mmoja wa wanamuziki walioleta mapinduzi makubwa ya muziki kutoka ule wa rhumba wa kina Franco na Tabu Ley na kuleta wa vijana ambao ulikuwa na mapigo ya kasi wao wakaita 'Cavasha'.

Hadi anafariki dunia, mwanamuziki huyo alikuwa akiishi nchini Uingereza, akiendelea na mambo ya muziki.

Alikuja nchini Tanzania miaka michache tu iliyopita akiwa mgeni wa mwanamuziki mwenzake Tshimanga Kalala Assosa ambaye walikuwa wote kwenye bendi ya Lipua Lipua, kabla ya kina Assosa na Nyboma kwenda kuunda bendi ya Les Kamale.

Ni mwimbaji mwenye sauti nzito, ambayo ukiisikiliza inashabihiana na ya Pepe Kalle au Madilu System.

Kutokana na kuishi nchini Uingereza, ambako kuna teknolojia kubwa zaidi, alikuwa ameshaanza kuziondoa nyimbo zake nyingi na bendi yake ya Lipua Lipua kwa mtindo wa Audio na kuziweka kwa mtindo wa video.

HADITHI

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe kutokuwa na msimamo, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja – 12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ZAHIR alinihitaji tu pale aliponihitaji. Hana kauli nzuri. Habembelezi, ana kiburi na maneno ya kashfa, dharau, kejeli na masimango. Nilivumilia, lakini nikashindwa. Nikarudi kwa Mashaka.

Ni kama nilikuwa nimefuga joka ambalo limenitafuna mwenyewe. Zahir hakutaka tena nirudi kwa Mashaka. Mapenzi yangu na Mashaka kwa mara ya pili yalikuwa ya kuwindwa. Hatukuwa na furaha tena.

Zahir akalipiza kisasi. Akamuua Mashaka bila sababu yoyote. Hili ndipo pigo kubwa kwenye maisha yangu. Kumuua Mashaka ni sawa na kuniua mimi. Lengo la Zahir ni kwamba amuue Mashaka ili nibaki na yeye.

Adui yake namba moja alikuwa Mashaka. Aliona akifa, basi pingamizi hakuna. Hakufikiri sawa sawa. Bora angeniua mimi angemuacha Mashaka wangu. Hakuwa na kosa lolote. Mimi ndiye mwenye makosa. Nasikitika sana, Mashaka amekufa kwa ajili yangu.

Taa yangu ya maisha imepotea. Nani atanipenda hapa duniani kama Mashaka? Nani atanijali? Nani ananidekeza. Nani atajali hisia zangu? Watakaosema wananipenda ni wengi. Lakini hawatakuwa kama Mashaka. Kwa sababu hiyo mimi nikaamua kuchukua jukumu. Jukumu zito. Jukumu ambalo sikufikiria katika maisha yangu kama nitakuja kulifanya.

Haiwezekani mtu aliyeniulia Mashaka wangu aendelee kuvuta pumzi ya dunia, wakati Mashaka ametulia tuli kaburini. Aendelee kula bata duniani, huku aliyemdhulumu nafsi yake akiwa futi sita chini ya ardhi. Nimeamua kumlipia kisasi. Mimi ndiye niliyemuua Zahir.

Ulikuwa waraka mrefu ulioandikwa na Cecilia. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni aliuonyesha mbele ya waandishi wa habari. Hii ni baada ya mtu mmoja aliyejuliaka kwa jina la Zahir kuuawa kwenye hoteli ya Coconut jijini Dar es Salaam.

"Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa kijana aliyeuawa kwenye hoteli hiyo, ameuawa na msichana aliyejulikana kama Cecilia, ambaye waraka huu tumeukuta nyumbani kwao Kinondoni." Alisema Kamanda.

Kamanda aliruhusu nakala ya waraka ule aupate kila mwandishi wa habari.




**"Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa kijana aliyeuawa kwenye hoteli hiyo, ameuawa na msichana aliyejulikana kama Cecilia, ambaye waraka huu tumeukuta nyumbani kwao Kinondoni." Alisema Kamanda.**

"Na nimemuua kwa sababu nilimchukia. Nilimchukia jinsi alivyonichukulia kama mwanamke. Alinichukulia mimi kama ni chombo cha kujifurahisha tu. Akanifanya nitoke kwa Mashaka, mwanaume aliyenipenda. Kibaya zaidi anakuja kumuua. Sijutii hata kidogo kumuua Zahir.

Ninachojuta ni kuidhulumu roho ya mtu ambaye hana kosa. Kosa lake nini? Kunipenda tu? Kwa kitendo cha kumuua Mashaka akidhani kuwa alikuwa kikwazo kwake alikosea. Ni kama kuniua na mimi pia. Ambacho alikuwa hafahamu ni kwamba mimi siwezi kuishi bila Mashaka.

Na ndiyo maana ilivyotokea baada ya Mashaka kuuawa nilichokuwa nikikitafuta ni ushahidi. Nilishiriki msiba nyumbani kwao hadi mwisho. Nilikuwa na wasiwasi na Zahir. Maneno yake mwenyewe yalimtia kwenye kitanzi. Ni mtu wa sifa, hivyo akanieleza kuwa kweli alimuua na alifanya hivyo kwa kutumia bastola ambayo amenionyesha.

Walimwengu, mimi ni mwanamke ambaye ni mwoga hata kuua nzi na sijawahi kuchinja hata kuku tangu nizaliwe, lakini alichofanya Zahir kilinitia hasira na ujasiri kwa hali ya juu, hivyo nilimuua mwenyewe kwa mkono wangu Coconut Hotel.

Nilimuua kwanza kwa ajili ya kulipa kisasi kwa mpenzi wangu Mashaka. Yeye amekufa, hivyo hakuwa na mtu wa kumlipizia kisasi. Na hata aliko huko atakuwa amefurahi kwa sababu si ndugu wala rafiki aliyemlipizia. Ni mimi mpenzi wake. Sasa atajua kuwa nilikuwa nampenda kiasi gani.

Kingine ni kuonyesha kuwa mwenye makosa ni mimi. Kitendo changu cha kumwacha kwa sababu ya tamaa na kutafuta mwanamume mwingine ndicho kilichomtia yeye matatani. Ningetulia na kupumzika naye, yote haya yansingetokea. Najuta.

Aliniita niende kwenye hoteli hiyo akitegemea kuwa sasa sina mtu yoyote ninayempenda zaidi yake. Nikachukua kisu changu nilichokuwa nimekinunua kwa sababu hiyo. Nikachukua na dawa za kulevya ambazo nilitumia kumuwekea kwenye kinywaji bila yeye kujua ili niifanye kazi hiyo kwa ufanisi zaidi bila kukosea, kwani mimi ni mwanamke. Chochote ambacho ningekosea na yeye kunyg'amua ingekuwa ni hatari kwangu, kwani sikuwa na msaada wa mtu yoyote.

Baada ya hapo nikarudi nyumbani. Nikaamua na mimi nijiue. Sina raha tena ya kukaa duniani. Nikae na nani? Niishi na nani? Na mimi nimejiua mwenyewe kwa kunywa idadi kunywa dawa ya kuua wadudu. Naombeni radhi wote kwa hili.

Naomba kwa ndugu zangu na watu wote na wa mpenzi wangu. Nizikwe pembeni mwa kaburi la Mashaka. Kama inawezekana tunaweza kuoana huko. Duniani imeshindikana.

Waraka ulikuwa imekomea hapo. Kamanda hakuwa na ufafanuzi zaidi kwa waandishi wa habari. Kila kitu kilikuwa kinajieleza.



# MARIOO USIZUNGUKE, SEMA UKWELI TU

STAA wa muziki wa Bongo Fleva, Marioo, ameipinga kauli ya msanii na bosi wa lebo ya Konde Gang, Harmonize, kuwa wimbo wake wa 'Ushamba' ni bora kuliko nyimbo zote za Novemba.

Marioo amesema Harmonize alitoa kauli hiyo wakati wimbo wake 'Mama Amina' ulikuwa haujatoka, vinginevyo maneno hayo yasingemtoka mdomoni.

"Wimbo wangu umetoka mwezi wa 11 una wiki sasa, kipindi kile anasema hivyo wimbo wangu ulikuwa bado haujatoka, kama ingetoka sidhani kama angeweza kuongea vile, dude langu hili ni kali na la moto kuliko magoma yote yaliyotoka sasa hivi" amesema Marioo.

## Balaa MC uliogopa gwaride la FFU

MSANII wa singeli, Balaa Mc, amesema aliogopa kushiriki video ambayo ilisambaa mitandaoni kipindi cha uchaguzi, ikiwaonyesha Askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) wakiwa wanaimba wimbo wake wa 'Nakuja'.

Akizungumza kupitia EATV, Balaa Mc amesema aliogopa kuposti kwani alihofia kufuatwa nyumbani, lakini baadaye akagundua kuwa ilikuwa ni sapoti ya watu kukubali kazi yake.

"Nilivyoona ile video niliogopa, kwanza nilimwambia hadi meneja wangu, niliogopa kwamba nisije nikaposti halafu wakanifuata nyumbani, ila niligundua wao wamekubali kitu ambacho nimekifanya, kuna mmoja kati ya wale kwenye kile kikosi alinicheki, nikakutana naye na tukaongea ninawashukuru sana" amesema Balaa Mc



## Stamina huyooo mdogomdogo

MSANII wa Hip hop anayeunda kundi la Rostam, Stamina, sasa ameamua kuanza safari yake peke yake baada ya kujiunga rasmi na lebo ya Akida OG.

Hatua hiyo imekuja siku chache baada ya msanii mwenzake, Roma Mkatoliki, hivi karibuni kuandika ujumbe ambao unaashiria anaweza kukaa pembeni na muziki.

Boss Akida OG, amesema ameamua kuchukua msanii huyo kwa sababu mke wake mkubwa anamfuatilia, kumpenda na kumtajataja.



## HABARI MICHEZO

# Scholes amtaka Pogba kumfukuza wakala

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa zamani wa Manchester United ambaye kwa sasa ni mchambuzi wa soka katika kituo cha BT Sport, Paul Scholes, ameeleza kuwa Paul Pogba anatakiwa kumzuia wakala wake, Mino Raiola, kutotoa maneno hasi kuhusu klabu hiyo.

Scholes amebainisha kwamba, Pogba anatakiwa kumfukuza wakala huyo kwani anamharibia.

"Sifikiri kama klabu inatakiwa kujibu hilo, kwa nini ampe wakala muda wa kufanya hivyo? Paul Pogba ndiyo tatizo kwa sababu anamlipa (Raiola) kumwakilisha yeye (Pogba), na (Raiola) anamwakilisha vibaya na Pogba ni mtu mzuri.

"Kila mmoja nje ya klabu atajua (Pogba) ndiyo ana matatizo kumbe siyo, (Pogba) ana vitu viwili tu vya kufanya juu ya Raiola, amwambie anyamaze au amfukuze kazi," amesema Scholes.

Kauli hiyo ya Scholes inakuja ikiwa ni siku mbili zimepita toka Mino Raiola atangaze kuwa Pogba hana furaha United na anataka kuondoka. Hii inakuja baada ya kiungo huyo wa Ufaransa kutopata nafasi ya kucheza sana kama zamani.

Nyota huyo inaelezwa kuwa anaweza kusepa ndani ya timu hiyo na kuibukia Klabu ya Juventus ambayo ilikuwa ni timu yake ya zamani.




# MESSI ASHAURIWA KUJIUNGA NAPOLI




**MANCHESTER,** England

KEVIN-Prince Boateng amemshauri nyota wa Barcelona, Lionel Messi kujiunga na Napoli kama sehemu ya kumwenzi gwiji wa Argentina, Diego Maradona.

Maradona ambaye anatajwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa soka wa wakati wote duniani, alifariki akiwa na umri wa miaka 60 kwa mshituko wa moyo mwezi uliopita.

Napoli imeuita uwanja wake Diego Armando Maradona kwa ajili ya kumwenzi mshindi hiyo wa Kombe la Dunia mwaka 1986, ambaye aliwaongoza miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kutwaa taji hilo mwaka 1987 na 1990 baada ya kutua hapo kutoka Barca mwaka 1984.

Messi alivua jezi yake ya Barca na kuonyesha ya Newell's Old Boys klabu ambayo Maradona alianza kuichezea soka, baada ya kufunga bao kwenye ushindi wa 4-0 katika mchezo wa LaLiga dhidi ya Osasuna msimu uliopita

Mchezaji wa zamani wa Barca, Boateng anataka mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi, ambaye amekuwa akihusishwa sana na Manchester City na Paris Saint-Germain, kufanya zaidi ili kumuenzi Maradona.

"Mara kwa mara nasikia kuhusu kulinganishwa Messi na Maradona na hivyo natuma ombi kwa Leo," alisema Boateng, ambaye kwa sasa anacheza katika klabu ya Serie B, Monza pamoja na Mario Balotelli, akiiambia ESPN.

# Garcia nje ya dimba kwa wiki tatu

**MANCHESTER,** England

ERIC Garcia atakuwa nje ya dimba kwa muda wa wiki tatu, amethibitisha Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Mlinzi huyo wa City amekuwa akihusishwa na timu kama Barcelona, Real Madrid na Arsenal baada ya kukataa kusaini mkataba mpya, alitolewa nje kipindi cha pili na nafasi yake kuchukuliwa na John Stones kipindi kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Marseille, Jumatano.

Garcia atakuwa nje ya dimba kwa wiki hizo tatu ingawa majeruhi yake hayajatajwa, lakini bosi wa City, Guardiola, amebainisha kwamba nyota huyo wa Hispania atalazimika kuwa nje ya dimba kwa muda, huku kiungo Ilkay Gundogan akionekana kuimarika.

"Eric Garcia hayupo fiti na atakuwa nje ya dimba kwa wiki mbili au tatu," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Awali tulidhani kwamba ameumia kwa kiwango kikubwa, lakini inaonyesha kwamba, atakuwa nje ya dimba kwa wiki chache tofauti tulivyofikiria.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AITABIRIA MAKUBWA MAN UNITED

●●● Rekodi ya kutwaa mataji inawasukuma huku akiamini wanaweza kutwaa EPL msimu...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anaamini Manchester United inaweza kushinda taji la Ligi Kuu England msimu huu.

**Kocha huyo wa United yupo kweye presha kubwa hasa ikizingatiwa timu yake imekuwa na matokeo yasiyoridhisha.**

Kikosi cha Solskjaer kipo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu (kabla ya mechi za jana) ikiwa imepitwa pointi tano na vinara Tottenham Hotspur.

"Ukiwa Manchester United, mara zote unatakiwa kuwa na malengo ya kushinda mataji," alisema Solskjaer, ambaye anaiongoza United ambayo haijashinda taji la Ligi Kuu tangu mwaka 2013.

"Bila shaka, kwa misimu mitatu iliyopita, kama ilivyo na kumekuwa na timu mbili zikiongoza kwa misimu kadhaa.

"Lakini naamini kwa msimu huu au tangu kuanza kwa mwaka huu, timu inaimarika na tunaweza kutoa changamoto kubwa kwenye kuwania taji msimu huu.

"Bila shaka tunahitaji kuimarika zaidi kuliko msimu uliopita, lakini sidhani kama tutashindwa kufanya vizuri, nina imani kubwa kwamba msimu huu ni wetu.

"Nakwenda katika kila mchezo nikiwa na malengo ya kushinda na huwa nina kuwa na hisia kwamba tunaweza kushinda."

## ZISIKUPITE

### BAYERN NA HUDSON-ODOI

BAYERN Munich haitamfuata winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi wakati wa dirisha la usajili la Januari, lakini mabingwa hao wa Ulaya wanaendelea kumfuatilia nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, raia wa England. ***(Goal)***

### HAALAND AWINDWA

TIMU za Manchester City na Manchester United zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### SZOBOSZLAI KUITOSA ARSENAL

KIUNGO wa Red Bull Salzburg, Dominik Szoboszlai mwenye umri wa miaka 20 raia wa Hungary, anapanga kuitosa Arsenal na atajiunga na RB Leipzig dirisha dogo la Januari. ***(Sky Germany via Sky Sports)***

### GRAY ATOSWA LEICESTER

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers amemwambia winga wa kimataifa wa England mwenye umri chini ya miaka 21, Demarai Gray hayupo kwenye mipango ya baadaye ya klabu hiyo. ***(Mail)***

### KOKE AMTAKA MESSI

KIUNGO wa Atletico Madrid, Koke, 28, amezungumzia kuhusu namna angependa kushawishi nyota wa Argentine, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33 kujiunga na Barcelona, lakini amekubali litakuwa jambo gumu kwa nyota huyo kuondoka pale ". ***(As)***

### WIJNALDUM KUTUA BARCA

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amebaki bado amatumaini ya kumsajili kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### CAVANI AIKATAA JUVE, INTER

STRAIKA wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 33, alikataa ofa za kujiunga na Juventus na Inter Milan na kuamua kutua Manchester United kwa uhamisho huru. ***(Sun)***

### LEICESTER, WEST VITANI

LEICESTER na West Ham zimeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Guinea, Amadou Diawara (23), ambaye anatarajiwa kuuzwa na klabu yake ya Roma. (***Leicester Mercury)***

### RENNES YAMKERA RAPHINHA

WINGA wa Leeds, Raphinha (23), amekiri alisikitishwa na uamuzi uliofanywa na klabu yake ya Rennes kwa kumuuza kwa klabu inayoshiriki Ligi Kuu England bila ya kumhusisha. ***(ESPN Brazil via Goal)***

### BURNLEY SOKONI

MCHAKATO wa kubadilisha umiliki wa klabu ya Ligi Kuu England ya Burnley wa thamani ya pauni milioni 200 kwenda kwa Kampuni ya Michezo ya Marekani unatarajiwa kukamilika wiki ijayo. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

## JKT Queens, Baobab zang'ara

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupokea kichapo kutoka kwa Simba Queens, 'Maafande' wa JKT Queens imezinduka kwa kuwafunga Mlandizi Queens mabao 5-1 katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Kwa matokeo hayo, JKT Queens sasa imefikisha pointi tisa na kurejesha matumaini ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo unaoshikiliwa na Simba Queens.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa juzi mchana kwenye Uwanja wa Jamhuri, Baobab Queens imewafunga ES Unyanyembe bao 1-0 wakati Alliance Girls iliyokuwa mwenyeji kwenye Uwanja wa Nyamagana imewafunga Ruvuma Queens mabao 2-1.

TSC Queens yenyewe ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mapinduzi Queens ya Njombe.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena Desemba 16, mwaka huu kwa Kigoma Sisterz kuwaalika JKT Queens wakati Yanga Princess itawafuata ES Unyanyembe huku Simba Queens ikivaana na Alliance Girls na Mlandizi Queens itawakaribisha TSC Queens.

Ruvuma Queens yenyewe itashuka dimbani kupambana na Baobab Queens na Mapinduzi Queens itakuwa nyumbani kuwania pointi dhidi ya Tanzanite Queens ambayo hivi karibuni itajulikana rasmi kwa jina la Fountain Gate Princess.

## JKU FC yajipanga kuiadhibu Mafunzo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa JKU, Omar Khamis 'Matu" amesema amejiandaa kuondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Mafunzo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa ..

Katika msimamo wa ligi hiyo, JKU iko kwenye nafasi ya pili kutoka mkiani mwa ikiwa na pointi moja baada ya kucheza mechi mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matu alisema licha ya kuanza vibaya katika ligi hiyo anaimani timu hiyo itaanza kupata matokeo mazuri katika mchezo wa leo baada ya kurekebisha upungufu aliouona kwenye michezo iliyopita.

Matu alisema kuwapo kwa uchache wa timu zinazocheza ligi hiyo msimu huu ikilinganishwa na msimu uliopita, imeongeza ushindani kwa sababu kila timu inataka kujiondoa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Wakati huo huo Black Sailor ilikubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa 'Maafande' wa Polisi katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Amaan huku katika Uwanja wa Mau B Wekundu wa Mjikongwe, Malindi pia walipoteza mchezo dhidi ya KVZ kwa kukubali kufungwa mabao 2-1 wakati Mlandege iliichapa Chuoni mabao 2-0.

# NAMUNGO YAJIPANGA KUWEKA HISTORIA CAF

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha linafika mbali kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, benchi la ufundi la Namungo FC linatarajia kuandaa programu maalumu ya kuwajenga nyota wake ili wafanye vyema kwenye michuano hiyo.

**Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemedi Morocco, aliliambia gazeti hili programu mpya ambayo ameiandaa itasaidia kurekebisha makosa ambayo ameyabaini tangu ajiunge na timu hiyo ya mkoani Lindi.**

Morocco alisema anaamini endapo wachezaji wake watafuata kikamilifu maelekezo yake, timu hiyo ina uwezo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na taji hiyo la Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza.

"Ninaendelea kufanyia kazi makosa ambayo nimeyaona katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na mchezo wetu wa kwanza wa Kombe la Shirikisho ambao tulicheza na klabu kutoka Sudan (Al Rabita FC), " alisema Morocco.

Kocha huyo aliongeza kwa sasa anawekeza nguvu zake katika mchezo huo wa kimataifa kwa sababu anataka kulitangaza vyema jina la Tanzania.

Hata hivyo, Morocco amewaomba mashabiki na wadau wa soka wa hapa kuipa ushirikiano timu hiyo ili ifanye vizuri na kufikia malengo makubwa waliyokuwa nayo.

"Hali za wachezaji wangu zipo vizuri na kila siku morali yao inaongezeka, tumejipanga kuhakikisha tunapata matokeo mazuri na kuweka historia mpya," alisema kocha huyo.

Kuhusu Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea, Morocco ameweka wazi mechi zote ni ngumu na kila mchezo kwao wanauona ni fainali.

Morocco alitua Namungo baada ya uongozi wa timu hiyo iliyocheza fainali za Kombe la FA dhidi ya mabingwa Simba kuamua kuachana na Thiery Hitimana.



Mshambuliaji wa Transit Camp inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, Hussein Nyamandugu 'Agogo', akimpiga chenga golikipa wa timu hiyo, Said Abdi, walipokuwa katika mazoezi kwenye Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Muhongo kurejesha mieleka Musoma*

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kufufua michezo mbalimbali ikiwamo ya mbio za mitumbwi, ngoma za asili na kwaya jimboni mwake, Mbunge wa Musoma Vijijini, mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo, amesema sasa anajipanga kutambulisha mchezo wa mieleka.

Muhongo alisema amefikia uamuzi huo kwa sababu mieleka ni moja kati ya michezo wenye mashabiki wengi ulimwenguni na umezidi kupata umaarufu, lakini pia upo michezo ya asili ambayo wenyeji walikuwa wakikusanyika na kushindana kama sehemu ya burudani.

Alisema anataka arejeshe enzi hizo ili kuendelea kuimarisha mshikamano, miongoni mwa wakazi wa jimbo hilo pamoja na wadau wa michezo na kuupa umaarufu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Kwa miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kufufua mbio za mitumbwi, kwaya na ngoma za asili, sasa rasmi tunageukia mieleka, ambayo kwa miaka mingi imepotea jimboni mwetu," alisema Muhongo.

Alieleza kila mwaka katika jimbo hilo kumekuwa na mashindano ya mbio za mitumbwi, kuimba, kucheza ngoma za asili, ambapo washindi hupewa zawadi za vikombe na fedha taslimu na sasa ameuongeza mchezo huo ili kuongeza hamasa.

"Kimsingi ni kwamba, mimi ni mdau wa michezo na nilishagawa vifaa vya michezo zikiwamo jezi na mipira katika vijiji, shule mbalimbali za msingi na sekondari jimboni hapa, ninaamini kupitia michezo tunajenga afya na kuimarisha mahusiano (uhusiano) ya wananchi," Muhongo aliongeza.

# Michezo

Jumapili Desemba 13, 2020

Nipashe




Solskjaer aitabiria makubwa United UKURASA 22

**KITU MKONO!...**



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Tuisila Kisinda, akiifungia Yanga bao la nne mbele ya mabeki wa Mwadui FC, katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa CCM Kambarage, Shinyanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga breki zimekatika*

## ●●● Yaipiga Mwadui mkono ikijitanua kileleni...

**Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza, vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wameweka rekodi ya kufunga magoli mengi zaidi kwa mechi moja katika msimu huu, baada ya kuichapa bila huruma Mwadui FC mabao 5-0. Mchezo huo uliofanyika katika Uwanja wa CCM Kambarage, Sinyanga, ulionekana kuwa wa upande mmoja.

**Mechi ambayo Yanga ilifunga mabao mengi ni dhidi ya Coastal Union ya Tanga ambayo iliibuka na ushindi magoli 3-0 Oktoba 3, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Kwa upande wa Mwadui FC, imekuwa ni kama ada kwao kupachikwa idadi kubwa ya mabao kwani, ilichapwa mabao 6-1 dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, Oktoba 25, mwaka huu, na Oktoba 30 ikabugizwa mabao 5-0 dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Yanga ilianza biashara asubuhi tu dakika ya tatu wakati Deus Kaseke alipofunga bao kwa staili ile ile anayofungana na pasi kutoka kwa Yacouba Songne, aliyempenyezea pande maridadi, mfungaji akawafungasha tela mabeki wa Mwadui na kuujaza wavuni na kuwa bao lake la tatu msimu huu.

Yacouba, raia wa Burkina Faso, akiwa kwenye kiwango cha hali ya juu, aliiandikia Yanga bao la pili dakika ya 13, akiunganisha krosi maridadi kutoka kwa Mukoko Tonombe.

Shambulizi pekee hatari zaidi kwa Mwadui kwenye mechi ya jana ilikuwa dakika ya 19, wakati Ismail Ally alipobaki na kipa Metacha Mnata, lakini shuti lake lilitoka nje kidogo ya lango na hali ikaenda hivyo hadi mapumziko.

Dakika nne tu baada ya mapumziko, Yacouba tena alipachika bao la tatu kwa Yanga, na la pili kwake kwenye mechi hiyo lakini pia likiwa ni la tatu kufunga kwa msimu huu.

Yalikuwa makosa ya mabeki wa Mwadui na kipa wao, Mussa Mbissa, yaliyomfanya mfungaji kuukwamisha wavuni akiwa amebaki na mabeki tu golini, kipa akiwa ameshatoka.

Mkongomani Tuisila Kisinda, alifunga bao lake la pili msimu huu kwenye Ligi Kuu dakika ya 56 na kuipatia Yanga bao la nne kwa shuti dhaifu la mguu wa kushoto, baada ya kupokea pasi kutoka kwa Yacouba aliyekuwa akihaha uwanja mzima.

Yanga iliwatoa Kaseke, Yacouba na Tuisila ambaye aliumia na nafasi zao kuchukuliwa na Haruna Niyonzima, Farid Mussa na Ditram Nchimbi.

Mabadiliko hayo yaliwaletea matunda dakika ya 69, wakati Farid alipoambaa na mpira na kumimina krosi ambayo ilimkuta Lamine Moro aliyeujaza wavuni huku mabeki wa Mwadui wakikaba kwa macho.

Kwa matokeo hayo, Yanga inaendelea kujichimbia kileleni, sasa ikiwa imefikisha pointi 37, ikishinda mechi 11 na sare nne, ikifunga mabao 22 na kufungwa mabao matano.

Hadi sasa, Yanga inaendelea kushikilia rekodi yake ya kuwa timu pekee ambayo haijapoteza mechi yoyote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

## Simba, Mbeya City vitani Bara

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya Dar es Salaam, wanatarajia kukutana na wenyeji Mbeya City katika mchezo wa ligi hiyo utakaofanyika leo kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini, Mbeya.

Simba itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata dhidi ya Polisi Tanzania, shukrani kwa Mzambia Clatous Chama aliyefunga magoli yote akitokea benchi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji, Sven Vandenbroeck alisema anahitaji kupata ushindi ili kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za kuwania taji hilo ambalo wanalishikilia kwa msimu wa tatu mfululizo.

Sven alisema mikakati yao ni kuhakikisha wachezaji wake wanapambana kutafuta pointi tatu ambazo zitawasogeza karibu na wapinzani wao ambao wana malengo ya kushinda taji hilo na kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa mwakani.

Kocha huyo alitaja malengo miwili waliyonayo msimu huu ni kutetea ubingwa na kufika mbali kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo wanashiriki msimu huu.

"Tuliwasili salama, wachezaji wapo tayari kwa mchezo, ninajua hautakuwa mchezo rahisi, utakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu wote tunahitaji kupata matokeo chanya, tunawaheshimu wapinzani wetu ambao wapo nyumbani lakini tuna kikosi imara ambacho kimekuja kutupatia matokeo mazuri," alisema Sven.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Wandiba alisema kikosi chake kimejipanga vizuri kukabiliana na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kinawahakikishia mashabiki wao watapata furaha.

Aliongeza wanafahamu mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa timu zote mbili na wamewatahadharisha Simba wasitarajie mteremko.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya JKT Tanzania dhidi ya Biashara United wakati Coastal Union itawakaribisha Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >